# Nipashe

Ijumaa Mei 1, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580220

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




TOLEO MAALUM

## ‘I Can, I Must, I Will’ kitabu kilichokonga nyoyo za wengi

UK. 3



Ijumaa Mei 1, 2020 Nipashe 11

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO, MHE. UMMY A. MWALIMU (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/2021

Mhe. Ummy Ally Mwalimu (Mb)
Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile (Mb)
Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

Prof. Mabula Daudi Nchembe
Katibu Mkuu (Idara Kuu Afya)

Dkt John Kiang'u Jingu
Katibu Mkuu (Idara Kuu Maendeleo ya Jamii)

UKURASA 11 - 15

TISHIO LA CORONA

# Wabunge wapinga utaratibu mazishi

**WATAKA** watu wazikwe kwao, washauri vituo zaidi upimaji, waziri aanika mikakati ya kuikabili, RC ajitangaza kupata maambukizo... *Uk. 2, 4, 5 & 7*



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiteta na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, bungeni jijini Dodoma, jana. **PICHA: OWM** .

## BAA LA CORONA



Kwa kuwa baadhi ya watu walio na maambukizo ya Covid -19 hawaonyeshi dalili, inashauriwa kuzingatia ukaaji kwa kuachiana nafasi hasa kwenye eneo ambalo ugonjwa huo umeshasambaa. WHO

- Epuka mikusanyiko ya watu
- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo

## DK. TULIA AONGOZA MAZISHI YA NDASSA

UKURASA 2

## Mwalimu jela miaka 30, achapwa viboko 24 kwa kubaka mwanafunzi

UKURASA 4





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play

Download on the App Store



MICHEZO KARIA: DK. MENGI ALITAKA KUIONA STARS QATAR 2022 UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, akitoa maelekezo kuhusu kilimo cha mpunga kwa viongozi wa Wilaya ya Magu alipotembelea Bonde la Kandawe kuangalia shughuli za kilimo cha mpunga jana, wakati wa ziara yake ya kukagua shughuli za maendeleo.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wabunge wapinga utaratibu wa mazishi

**Na Salome Kitomari,**
DODOMA

UGONJWA wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona, jana ulitawala mjadala wa Bunge, huku baadhi ya wabunge wakitaka watu kuruhusiwa kuzika wapendwa wao tofauti na hali ilivyo sasa.

Mbunge wa Kigoma Kusini (CCM), Hasna Mwilima, alisema pamoja na kazi nzuri inayofanyika katika kukabiliana na corona, ni vyema watu wakaruhusiwa kusafirisha wapendwa wao na kuwazika kwenye familia zao kuliko kuzikwa kokote.

"Mtu asafirishwe azikwe kwenye familia yake na si kuzikwa kokote. Naomba sana machungu yaliyopo kwa waliopoteza ndugu zao ni namna watu wanazikwa tu na si katika maeneo wanayoyataka wao," alisema. Baada ya Mwilima kumaliza kuchangia, Spika Job Ndugai alisema serikali iangalie jambo hilo kwa kuwa litasababisha madhara makubwa baadaye.

"Unajua hili suala la maziko limetutatiza, kwa Mchungaji Getrude Rwakatare tulisimama wima akazikwa sehemu familia iliyotaka na wanakwenda kuzuru kaburi na Richard Ndassa hivyo hivyo wanalala mahala pale familia zimetaka," alisema.

Alisema tatizo hilo lisipoangaliwa vizuri, baadhi hawatapelekwa hospitalini kwa kuwa wanaamini wakimpeleka mbali na kupata huduma za afya akapona lakini ikitokea akafa hawatapewa mwili, hivyo wataona bora akae nyumbani afe hapo na wamzike wenyewe. Aidha, mjadala huo ulitawaliwa na suala la uhaba wa vifaa kwa watumishi wa afya ikiwa kupewa motisha kwa kuongeza fedha, pamoja na kuweka vituo vya kupima kila mkoa kuliko sampuli kusafirishwa hadi Dar es Salaam.

Mbunge wa Mbeya Mjini (Chadema), Joseph Mbilinyi, alisema bajeti (makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto) hiyo imekuja kama vile hali ni kawaida wakati watu wanakufa na kwamba taarifa zinakuwa nyingi za kutisha watu.

Mbunge wa Mtwara Vijijini (CCM), Hawa Ghasia, alisema watumishi wa afya wanaofanya kazi kwenye janga la corona wapate posho ya kuwangezea morali ya kufanya kazi zao kuliko kuendelea kuwalipa stahiki zao za kila siku.

Naye Mbunge wa Viti Maalum (CUF), Sonia Magogo, aliitaka serikali kuwekeza katika vipimo ili watu wengi waweze kupima watu wengi, na kwamba wauguzi wanakimbia wagojwa kutokana na uhaba wa vifaa na uhakika wa afya zao. Kuhusu mabasi ya mikoani, alisema abiria walazimishwe kuvaa barakoa kwa sababu wanakaa muda mrefu huku akitolea mfano wa ndugu yake aliyesafiri wakati wanatoka Dar amevaa barakoa ila walivyofika Chalinze walizitoa na alivyofika aendako akapimwa na kukutwa na maambukizo.

Naye Mbunge wa Kawe (Chadema), Halima Mdee, alitaka Serikali kutoa fedha zote zilizopangwa mwaka huu ili kuiwezesha kupambana na Corona, kuliko kuendelea kuipa fedha kama wizara nyingine.

"Tuliunda kamati ili Serikali ilete taarifa bungeni lakini leo ni mwezi mzima hatujui kinachoendelea, hatujaambiwa tuje hapa kushauri tu bali kuisimamia Serikali kwa mujibu wa katiba," alisema.

# Dk. Tulia aongoza mazishi ya Ndassa

**Na Salome Kitomari,**
DODOMA

NAIBU Spika, Dk. Tulia Akson, ameongoza msafara wa mazishi ya aliyekuwa Mbunge wa Sumve, Richard Ndassa (61), aliyefariki dunia juzi jijini hapa.

Kabla ya kuanza kwa kikao cha Bunge jana, Spika wa Bunge Job Ndugai, aliwaeleza wabunge kuwa mwili wa mbunge huyo ulisafirishwa juzi usiku na kuzikwa jana jioni kijijini kwake.

Wabunge waliwakilishwa na Mbunge wa Sengerema (CCM), William Ngeleja. "Niwataarifu mwili wa Ndassa ndio umewasili pale Sumve muda huu (jana saa nane na robo) kwa hiyo jioni hii mazishi yatafanyika, waliondoka saa sita usiku wa kuamkia leo (juzi) tumewakilishwa na Ngeleja na Naibu Spika, tunawatakia kila heri katika jambo hilo wanalotuwakilisha," alisema Spika Ndugai.

Juzi, akitangaza kifo cha mbunge huyo, alisema wanawasiliana na serikali pamoja na familia kuhakikisha mbunge huyo ambaye amedumu bungeni kwa kipindi cha miaka 25, anazikwa jimboni kwake na si kokote.

# Bunge lataka vituo zaidi upimaji virusi vya corona

**Na Salome Kitomari,**
DODOMA

WABUNGE wameitaka serikali kuongeza vituo vya upimaji wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (COVID-19) katika hospitali za kanda nchini ili huduma itolewe kwa haraka na kwa watu wengi.

Akiwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii jana bungeni, Mwenyekiti Peter Serukamba, alisema iwapo upimaji utafanyika, utapunguza kusambaa kwa ugonjwa huo nchini.

Pia alishauri serikali ichukue hatua za dharura za kuongeza vifaa kwa ajili ya madaktari na wauguzi ili kuwakinga na ugonjwa huo wakati wakitoa huduma kwa wagonjwa.

"Fedha zitumike kuhakikisha uwapo wa vifaa tiba kama vile 'Oxygen concentrators', 'ventilators', pamoja na madawa (dawa)," alisema.

"Kamati inawataka wananchi kutekeleza kwa vitendo ushauri na elimu inayotolewa na serikali juu ya namna bora ya kujikinga na ugonjwa huu. Ni ukweli ulio wazi kuwa endapo jamii itazingatia ushauri na elimu hiyo, basi maambukizi yatapungua kwa kiasi kikubwa," alisisitiza.

Serukamba pia alisema ni vyema serikali ikaimarisha mifumo ya afya kama ilivyoainishwa katika mihimili sita iliyopendekezwa na Shirika la Afya Duniani (WHO). Alitaja mihimili hiyo kuwa ni utoaji wa huduma za afya, rasilimali watu; utawala bora katika masuala ya afya; dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi; na ugharimiaji wa huduma za afya na mifumo ya takwimu.

"Ni dhahiri mifumo hii ikiimarishwa italeta matokeo chanya katika kukabiliana na kuthibiti maambukizi ya corona," alisisitiza.

Serukamba aliwataka Watanzania kuendelea kumuomba Mungu kulingana na imani zao ikiwamo kutumia njia mbadala na za asili kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa huo.

"Ni matumani ya kamati kuwa, serikali itatoa motisha kwa wahudumu wa afya kama vile 'risk allowance' (posho ya mazingira magumu), 'extra duty allowance' (posho za kazi za ziada) ili kuwapa morali (ari) ya kuendelea kufanya kazi katika mazingira haya magumu," alisema.

Serukamba alisisitiza kuwa katika mapambano dhidi ya corona ni muhimu sekta zote na jamii kwa ujumla zikashirikiana kikamilifu.

Naye Waziri Kivuli mwenye dhamana ya afya kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Cecilia Paresso, alisema utoaji wa taarifa kwa umma kuhusu mwenendo wa maambukizi ya corona unatiliwa shaka kwa kuwa Watanzania wengi wanaendelea kujiuliza usahihi wa taarifa hizo na kama kuna uwazi wa kutosha juu ya idadi halisi ya watu walioambukizwa na idadi ya vifo.

"Serikali haipaswi kuficha chochote, ni vyema ikatambua kuwa taarifa za vifo na idadi ya watu walioambukizwa zinapatikana kupitia familia na ndugu wa wahusika. Hata hivyo kupitia mitandao ya kijamii tunaona na kusoma ujumbe mfupi wa maandishi kutoka familia mbalimbali zikieleza kuhusu wapendwa wao kupata maambukizi na au kupoteza maisha.

"Ukiweka mzani wa mlinganisho wa taarifa hizo na taarifa ya serikali ni dhahiri kuwa kuna tatizo mahali ya kuficha takwimu halisi za watu waliopata maambukizi na waliofariki (dunia)," alisema na kuongeza:

"Jambo la kusikitisha zaidi waliofariki (dunia) wanazikwa usiku kwa usiku huku kukiwa na timu maalum zilizoandaliwa na magari ya kutosha. Tunajiuliza nguvu hiyo inayotumika kwa nini isingetumika kuokoa maisha ya wagonjwa hao? Ni vyema viongozi mkakumbuka kuficha au kufanya siri jambo linalogusa uhai wa watu ni hatari sana na linapaswa kupingwa kwa nguvu zote."



## DK. REGINALD ABRAHAM MENGI

"Unaweza kubadilisha maisha yako endapo utakuwa na imani ya dhati ya vile unavyotaka kuwa."

# I Can, I Must, I Will: Kitabu kilichokonga nyoyo

**Na Michael Eneza**



Rais John Magufuli akikata utepe kuzindua kitabu cha I Can, I Must, I Will


ALIPOANDIKA kitabu cha maisha yake, Dk. Reginald Mengi hakuwa na habari kuwa kwa upande mmoja alikuwa anawausia vijana na hata baadhi ya watu wa kizazi chake na kichofuata, kuhusu siri ya mafanikio yake. Huwezi kusema kuwa alitoa siri zote za mafanikio yake katika kitabu cha 'I Can, I Must, I Will,' lakini kimsingi alidhihirisha kuwa dhamira ni jambo la msingi sana katika maisha. Bila dhamira iliyo imara mtu hawezi kusimama kwa muda mrefu katika uelekeo fulani, ayumbishwe na mitikisiko ya hapa na pale, akate tamaa.

Profesa mmoja wa masuala ya kimataifa Chuo Kikuu cha Bordeaux I (sasa marehemu) aliasa katika darasa (wanaita mhadhara) mwisho wa mwaka 1985 kuwa mtu akishafikia umri wa miaka 35 hawezi kubadilika tena. Ina maana kuwa mwelekeo wa maisha unaandaliwa wakati mtu yuko katika ujana, akishavuka kipindi hicho hawezi tena kuelekezwa njia moja au nyingine, labda iwe ni nidhamu ya woga. Kujifunza kikamilifu kimsingi kunaendana na kipindi cha ujana, mtu anapojenga msingi wa kimawazo wa kukabili matatizo, hisia ya ufanisi wa kuyatatua.

Watu waliosoma kitabu hicho na kufanya mapitio katika mitandao waliunganishwa na 'habari' moja ya msingi, kuwa "this is a powerful account of the story of Africa told through the life of one of its contemporary shapers, Reginald Abraham Mengi of Tanzania. I Can, I Must, I Will comes at a time when Africa is casting a new vision that is guided largely by the power of entrepreneurship." Siyo rahisi kuboresha kilichosemwa hapo, kuwa ni kitabu hasa cha picha na sura ya Afrika katika kipindi cha kujinasua kutoka utegemezi kwa serikali, kuingia hatua ya ujasiriamali kwa sehemu isiyo ndogo ya jamii. Dk. Mengi alikuwa mfano, siyo tu wa kuigwa ila hata kuiga ni kazi ngumu; ndiyo maana watu wanasoma kutafuta siri za ujasiri huo.

Wasomaji hao wako wa aina mbili, kwa msingi wa mhadhiri huyo wa Ufaransa, wale ambao tayari maisha yao yameshachukua mwelekeo ambao hawezi kubadilishwa kwa kujifunza hiki au kile, na wale ambao bado wanajifunza. Wengi wao ndiyo walioko au walikuwa katika vyuo na vyuo vikuu wakati kitabu hicho kinachapishwa mwaka 2018, na kwa sehemu kubwa ndiyo wenye uwezo wa kutafakari ujumbe wake, kupata mbinu za kujijenga kimaisha na kibiashara. Uelekeo wa mtu kimaisha haujengwi na kitu kimoja ila mchango wa maana unaweza kuelekeza mawazo au akili ya mtu katika uelekeo unaohitajiwa, akichuja yaliyokuwapo awali, abadilike.

Unaweza pia kusema kuwa kitabu hicho kiliendana na jitihada za kupambanua sera zinazofaa katika kustawisha uchumi wa nchi, kati ya mwelekeo wa kidola unaosisitiza ufanisi wa sekta ya umma na usimamizi wa nguvu wa sekta binafsi. Kwa upande fulani mwelekeo huo unatokana na historia ya Tanzania katika awamu ya kwanza, kuona wafanyabiashara kama wahujumu uchumi. Hisia hiyo haijamalizika na kwa maisha yake, siyo tu kufaulu ila kuwajali wengine, Dk. Mengi alibadili sura ya mfumo wa soko ikawa ni eneo ambako Waafrika wanaweza, si kuonewa.





Kitabu kilichotungwa na Dk Mengi

Mfano wa Dk. Mengi kama mbunifu na mjasiriamali aliyeangalia na kuona kuna kitu hakipo kwenye soko inabidi kupatikane ulichangamsha hisia za Waafrika kila mahali

Mfano wa Dk. Mengi kama mbunifu na mjasiriamali aliyeangalia na kuona kuna kitu hakipo kwenye soko inabidi kupatikane ulichangamsha hisia za Waafrika kila mahali. Wakati mmoja (mwaka 2004) aliyekuwa Waziri wa Elimu nchini Zimbabwe, Dk. Jonathan Moyo, aliuambia mhadhara Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (ilikuwa ni wakati wa likizo, hapakuwa na wahudhuriaji wengi) kuwa akirudi nyumbani angeandaa ujumbe wa vyombo vya habari vya Zimbabwe na Afrika Kusini kuja Tanzania. Sababu ni kufika IPP Media na kujionea wenyewe, wathibitishe kuwa 'kumbe inawezekana' kwa Waafrika nao kuwa vyombo vikubwa vya habari.

Ukichukulia hisia hiyo kutoka kwa waziri wa Zimbabwe unapata picha ya upana wa kustaajabu na kutaka kujua uwezo huo ulipotokea, na kwa vile bado ni mapema tangu ameondoka kati yetu, ni wazi kuwa kitabu hicho kitaendelea kutafutwa na vijana wa rika la vyuo na vyuo vikuu. Hata miongoni mwa wajasiriamali wengine waliokuwepo wakati huo, miaka ya 1980 mwishoni, siyo rahisi kupata waliofanikiwa kwa mwelekeo kama wa Dk. Mengi. Tofauti yake na wengine ni kuwa hakujikita katika fani moja na kuishia hapo ila alithubutu kuingia katika fani tofauti na kimsingi alifaulu kote. Aliachia kampuni au shughuli idondoke kama hana hamasa nayo tena, iwe ni kwa sababu faida yake inapungua au atumie muda wake kwingine zaidi kwa wakati huo.

Yako maeneo ambayo baadhi ya vijana wa vyuo na vyuo vikuu watakuwa wameanza kujifunza kutoka katika kitabu hicho, na hata ingebidi 'kujiongeza' kwa kiasi fulani baada ya kusoma kitabu au kupata picha ya mtiririko wake kimsingi. Mojawapo ni ulazima wa kujenga rasilimali mtu akiwa bado kijana, wakati ana nguvu zaidi za kufanya kazi na nyakati tofauti anaweza kuwa mshauri katika maeneo tofauti. Pesa katika maisha haziji kila wakati, lakini zinapotokea katika mazingira haya au yale inabidi zitumike vizuri, si kwa kuweka benki bali kwa kuwekeza Dk. Mengi alitumia ujana wake na kipato chake kama mtaalamu wa uhasibu kuweka msingi wa uwekezaji (tofauti na ujasiriamali wa kawaida) nyakati zilipobadilika uwekezaji ukaanza kuthaminiwa. Ilikuwa ni kujikumbushia alichojifunza awali kwa Mwalimu Nyerere,'it can be done if you play your part.'



Rais John Magufuli akizindua kitabu cha I Can, I Must, I Will kilichotungwa na Dk Reginald Mengi. Kushoto ni Rais Mstaafu Ali Hassan Mwinyi.

# Mwalimu jela miaka 30 kwa kubaka mwanafunzi

**Na Manuel Kaminyoge,**

ILEJE

MAHAKAMA ya Wilaya ya Ileje mkoani Songwe, imemhukumu kutumikia kifungo cha miaka 30 jela na kuchapwa viboko 24 Abed Rajab Mbuba (54), ambaye ni mwalimu wa Shule ya Msingi Shinji iliyopo Kijiji cha Shinji, kata ya Mbebe kwa kosa la kumbaka mwanafunzi.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Shughuli Mwampashi, alisema

mtuhumiwa alitenda kosa hilo Julai, 2019 katika maeneo ya kijiji Cha shinji kwa kumbaka mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Shinji, huku akijua kufanya hivyo ni kosa na ni kinyume cha kifungu cha sheria namba 130 kifungu kidogo

cha kwanza na pili E na kifungu cha 131.

Mwampashi alisema mahakama hiyo baada ya kusikiliza pande zote mbili, imeridhika na ushahidi upande wa mashitaka, na kumhukumu mtuhumiwa kutumikia kifungo cha miaka 30 jela na kucharazwa viboko 30 ili liwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia kama hizo.

Awali Mwendesha Mashitaka, Peter Mrisho, aliomba mahakama kutoa adhabu kali kwa mtuhumiwa kwani vitendo vya ubakaji vimekithiri wilaya ya Ileje, ambapo husababisha kukatisha ndoto za wanafunzi kwa kuwapa mimba.

Akitoa utetezi wake, mshitakiwa alidai ana familia inayomtegemea, hivyo akihukumiwa familia itakosa mwelekeo, na kuiomba mahakama impunguzie adhabu.

Hata hivyo, Hakimu Mwampashi alitupilia mbali ombi hilo, na kuamuaru akatumikie kifungo cha miaka 30 jela na kuchapwa viboko 24.




TANESCO

Tunayaangaza maisha yako

MEI MOSI 2020

Bodi ya Wakurugenzi, Uongozi na Wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), tunaungana na Watanzania wote katika maadhimisho ya

Sikukuu ya Wafanyakazi, Mei Mosi

Piga kupitia simu namba +255 222 194 400 na +255 768 985 100

"TANESCO Tunayaangaza maisha yako"

tanesco_official_page umemeforum.blogspot.com tanescoyetultd tanescoyetu


## RC ajitangaza kuambukizwa corona

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, amejitangaza kuwa amepata maambukizo ya virusi vya corona baada ya kuamua kupima afya yake kwa hiari bila ya kuwa na dalili zozote.

Dk. Mghwira alithibitisha hilo juzi, akibainisha kuwa baada ya mizunguko mingi ya kufuatilia mwenendo na hali ya maambukizo ya corona mkoani mwake na kukutana na makundi mengi ya wananchi, aliamua kupima afya yake.

"Niliona ni vizuri kupima ili kuangalia afya yangu, niliamua kufanya hivyo kwa sababu kazi yangu inaingiliana na watu.

"Nimepima na matokeo yameonyesha nimeambukizwa virusi vya corona. Sina dalili za corona, sina homa, wala sina chochote isipokuwa vipimo vimeonyesha hivyo," alisema.

Kiongozi huyo wa mkoa alisema watu wengi wanaweza wakawa wanatembea huku wakijiona wapo salama kumbe wana maambukizo, hivyo akawataka wapime kwa hiari kwa sababu ni muhimu.

Aliwaomba wananchi wa mkoa huo wazingatie masharti yanayotolewa na wataalamu wa afya kujinga na maambukizo ya virusi hivyo.

"Sokoni bado watu hawajazingatia uvaaji wa barakoa, watu wanakaa karibu, nilipokuwa nikienda kwenye makundi ya watu, nilikuwa naona kuna kitu kinaniingia, kikawa kinanipa hisia kuna tatizo," alisema.

Dk. Mghwira alisema uzoefu wake mfupi wa kuishi na maambukizo hayo, umempa somo kuona kuna tija kwa wagonjwa kutunzwa nyumbani kuliko kwenye vituo.

"Ninasema hivi kwa sababu, kama mwanafamilia mmoja ameambukizwa nje au ndani, uwezekano wa kuambukiza wanafamilia ni mkubwa.

"Tukianza kutunzana nyumbani, itapunguza gharama na kusaidia kuimarishana kama familia kuliko mmoja akitengwa, ni kitu kigumu sana.

"Nimejaribu hapa katikati kuwaonyesha watu wote waliokuja karibu na mimi kwamba nimepima. Je, ikija nina maambukizo, unaonaje haiwezekani tu, huwezi ukawa umeambukizwa halafu uwe hivi, sasa niweje? Tunahitaji kujifunza kupokea mambo magumu," alishauri.

Dk. Mghwira ni kiongozi wa kwanza kujitangaza kupata maambukizo ya virusi hivyo nchini tangu serikali iliporipoti mgonjwa wa kwanza Machi 16 mwaka huu.



Mwezeshaji wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kujikinga wakati wa kuwahudumia wagonjwa wa Covid 19, kutoka Halmashauri ya Ushetu, Athanas Lucas, akiwaelekeza wataalamu wa afya (hawapo pichani), namna ya kuvaa mavazi maalum kwa ajili ya kuwahudumia washukiwa na wagonjwa wa virusi vya corona. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Wizara yaanika mikakati kukabili virusi vya corona

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

SERIKALI imesema imetoa mafunzo ya kukabiliana na ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona (Covid-19) kwa wataalamu wa afya 2,113 wa mikoa 11 nchini.

Vilevile, imesema imeimarisha uwezo wa kupima sampuli kwa watu wote wanaohisiwa kuwa na viashiria au dalili za ugonjwa huo, ikibainisha kuwa kwa sasa Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii imejengewa uwezo kwa kupatiwa mahitaji yote muhimu katika kupima virusi.

Akiwasilisha bungeni jijini hapa jana, makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alisema serikali imekamilisha ujenzi na uungaji wa vifaa katika jengo jipya kwa ajili ya kukabiliana na corona.

Alisema watumishi 120 wameajiriwa kwa muda ili kuimarisha ufuatiliaji wa wasafiri wanaoingia nchini kupitia maeneo ya mipakani na kwamba serikali imeandaa utaratibu maalum wa kuwaweka chini ya uangalizi wa siku 14 kwa gharama zao.

Waziri Ummy alisema upande wa huduma za matibabu kwa wagonjwa, serikali inaendelea kuwapatia matibabu wagonjwa wa corona na kwamba kwa Dar es Salaam, matibabu yanatolewa katika Kituo cha Magonjwa Hatari ya Kuambukiza Temeke, Kisoka-Mlonganzila na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Amana.

Alisema serikali pia inajenga kituo cha kisasa cha wagonjwa wa magonjwa hatari ya kuambukiza eneo la Kisoka-Mloganzila, Dar es Salaam.

"Makatibu tawala wa mikoa na wilaya zote Tanzania Bara wameelekezwa kuandaa maeneo maalum kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa katika mikoa endapo watajitokeza katika maeneo yao. Hadi Aprili 24 April, mwaka huu, jumla ya mikoa 17 ina vituo vya matibabu ya wagonjwa wa corona," alibainisha.

Waziri huyo alisema mafunzo ya watumishi yametolewa katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Kilimanjaro, Arusha, Rukwa, Songwe, Tabora, Dodoma, Tanga, Mbeya na Pwani na yanaendelea kwa mikoa iliyobaki.

Alisema wizara yake pia imeendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya namna ya kujikinga na kutambua dalili za ugonjwa huu. Elimu hiyo imeendelea kutolewa kwa njia ya vyombo vya habari (magazeti, redio na runinga), mitandao ya kijamii, shuleni, vyuoni, nyumba za ibada na vyombo vya usafiri.

"Nawashauri wananchi kwa kuzingatia maelekezo mbalimbali tunayowapatia ikiwamo kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka na kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima.

"Tunaendelea kuwakumbusha Watanzania kuwa ugonjwa huu ni wa hatari na hauna kinga wala tiba, na njia pekee ya kujikinga na ugonjwa huu ni kufuata maelekezo ambayo yamekuwa yakitolewa na wataalamu wa afya kuhusu namna bora za kujikinga na ugonjwa huu," alisema.

Waziri Ummy alisema katika kudhibiti na kuhakikisha kuwa ugonjwa huu hauathiri watu wengi zaidi, serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuimarisha ufuatiliaji wa wasafiri wanaoingia nchini kupitia viwanja vya ndege, bandari na mipaka ya nchi kavu ili kuweza kubaini wanaoonyesha dalili za ugonjwa.

"Hadi Aprili 24, 2020, jumla ya wasafiri 2,001,670 wamepimwa joto la mwili (thermol screening) ili kubaini kama wana homa ikiwa ni dalili za awali za ugonjwa huu na wasafiri 3,064 waliweza karantini katika maeneo mbalimbali hapa nchini kati yao 2,101 wamekamilisha muda wa siku 14 na kubainika kuwa hawana maambukizo na hivyo kuruhusiwa kuendelea na shughuli zao za kawaida," alifafanua.

Waziri huyo alisema katika kuhakikisha kuwa wasafiri wote wanaoingia nchini wanapimwa joto la mwili, serikali imenunua jumla ya vipimajoto 324 (vya mkono 307 na vya kupima watu wengi kwa mpigo 17) ambavyo vimefungwa na vinatumika katika maeneo ya mipakani ikiwamo viwanja vya ndege na bandari.

Corona iligundulika Desemba 31 mwaka 2019 katika Jimbo la Wuhan, China na hadi sasa watu 480 wameugua nchini, 16 wamefariki dunia na waliopona ni 197, na watu 283 wanaendelea na tiba kati yake 14 wako chini ya uangalizi.

Duniani watu zaidi ya milioni tatu wameambukizwa na kati yao, zaidi ya 200,000 wamefariki dunia katika nchi na maeneo ya utawala 185.

# Polisi yaendelea kuwashikilia Wakili Msando, mwandishi

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

JESHI la Polisi mkoani hapa limeendelea kumshikilia wakili maarufu Albert Msando, mkazi wa Lemara jijini hapa kwa zaidi ya saa 27 kwa madai kuwa halijakamilisha mahojiano kuhusu madai ya uchochezi dhidi ya serikali kuhusu ugonjwa hatari wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona (Covid-19).

Habari za kushikiliwa kwa wakili huyo na polisi zilizagaa kwenye mitandao ya kijamii juzi. Hata hivyo, Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Arusha, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Koka Moita, alithibitisha hilo kwenye mkutano wake na waandishi wa habari uliofanyika katika makao makuu ya jeshi hilo jana.

Alisema polisi inamshikilia kufuatia 'Clip' iliyosambazwa baada ya kufanya mkutano na waandishi wa habari mkoani Arusha kwa malengo ya kuwagawia vidhibiti vya ugonjwa wa Covid-19 na kudaiwa kusema 'hali ni mbaya sana juu ya ugonjwa huo', wakati hana mamlaka ya kuzungumza lolote kuhusu ugonjwa.

"Ukweli ni kwamba na niseme bila kuficha hali ni mbaya kwa Arusha na ndugu waandishi nyinyi ni lazima mfike mahali muweke miguu chini mseme ukweli ili wananchi, serikali na kila anayehusika atambue kwamba tupo katika hali mbaya, ambayo kila mmoja wetu anapaswa kuchukua hatua, mkirudi nyuma na kuogopa kusema tutazikana," Kaimu Kamanda Moita alinukuu maneno anayodai ni ya Msando kwa waandishi wa habari. Alisema polisi ilimkamata juzi na mahojiano na wakili huyo yanaendelea.

Alisema polisi wamechukua hatua hiyo kutokana na Msando kukiuka maelekezo ya serikali kuwa wenye mamlaka ya kutoa taarifa za ugonjwa huo ni Waziri Mkuu, Waziri wa Afya na Msemaji Mkuu wa Serikali.

Pia, polisi mkoani Arusha inamshikilia Agness Shinji, mkazi wa Lemara kwa tuhuma za kusambaza taarifa za uongo mitandaoni.

Kaimu Kamanda Moita alisema Aprili 9, mwaka huu mtuhumiwa akitumia grupu la Whatsapp liitwalo 'Football for life' alituma taarifa kuwa mtangazaji wa Shirika la Utangazaji la Taifa TBC1, Gloria Maiko amefariki dunia kutokana na ugonjwa wa corona jambo ambalo si kweli na kusababisha taharuki kwa ndugu jamaa na marafiki.

Alisema baada ya jeshi kubaini kuwa ni uzushi lilianza kumfuatilia Agness na Aprili 29, alikamatwa na amekubali kulifahamu tukio hilo la kutuma taarifa za kifo cha mtangazaji huyo bila ya kuwa na uhakika.

Moita alisema watuhumiwa wote wawili watafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika ili sheria ichukue mkondo wake. Kaimu Kamanda Moita alitoa onyo kwa makundi yote wakiwamo viongozi wa siasa na wananchi kwa ujumla kutokuwa wasemaji wa serikali na wanapaswa kutii amri na maelekezo yanayotolewa na viongozi wakuu wa serikali badala ya kukaidi kwa kuwa kufanya hivyo ni kosa kisheria.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KISUTU**
**DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA MADAI NO** 13 **YA MWAKA 2020**

M. M INDUSTRIES LTD ..................... **MDAI**

**DHIDI YA**

ELCAT BUILDERS (T) LTD ..................... **MDAIWA**

**KWA:**
The Managing Director, ELCAT BUILDERS (T) LTD.
P.O. Box 21029
DAR-ES SALAAM

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya mdai yameelezwa katika nakala ya madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo Mnahitajiwa kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au kwa Wakili au mwakilishi ambaye anaruhusiwa, siku ya tarehe 12/05/2020 saa **01.00. mchana**

**ANGALIA:**
Kama hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama mmepokea kuitwa shaurini, itaweza kutoa hukumu kuwa mmeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 15/04 **2020.**

**HAKIMU MKAZI MKUU**
**KISUTU -DAR ES SALAAM**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ushauri wa wabunge kwa serikali corona uzingatiwe

**WABUNGE** wameitaka serikali kuongeza vituo vya upimaji wa virusi vya corona (Covid-19) katika hospitali za kanda nchini, ili huduma itolewe kwa haraka na kwa watu wengi.

Akiwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu Huduma na Maendeleo ya Jamii, jana bungeni, Mwenyekiti Peter Serukamba, alisema upimaji utafanyika, utapunguza kusambaa kwa ugonjwa huo nchini.

Aidha, serikali ichukue hatua za dharura za kuongeza vifaa kwa ajili ya madaktari na manesi, ili kuwakinga na ugonjwa huu kipindi hiki wanachotoa huduma kwa wagonjwa.

Kadhalika, wabunge walisema ni vyema serikali ikaimarisha mifumo ya afya kama ilivyoainishwa katika mihimili sita iliyopendekezwa na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Aidha, iliishauri serikali kutoa motisha kwa wahudumu wa afya ili kuwapa morali ya kuendelea kufanya kazi katika mazingira magumu. Walisema katika mapambano ya corona ni muhimu sekta zote pamoja na jamii kwa ujumla wake kushirikiana kikamilifu.

Kimsingi, tunakubaliana kabisa na ushauri wa kamati kwa serikali kuongeza vituo vya upimaji wa virusi vya corona katika hospitali za kanda nchini, ili huduma itolewe kwa haraka na kwa watu wengi.

Tunasema hivyo kwa kuwa hatua hiyo itawawezesha watu wengi kupima, hivyo kupunguza uwezekano wa maambukizi kuongezeka. Pale watu wanapopima na kupata majibu, inakuwa rahisi kuanza kupatiwa matibabu, huku pia wakiwa mbali na watu wengine, ambao wangeweza kuwaambukiza.

Tunaunga mkopo pia ushauri wa kamati kwa serikali wa kuchukua hatua za dharura za kuongeza vifaa kwa ajili ya madaktari na manesi, ili kuwakinga na ugonjwa huu kipindi hiki wanachotoa huduma kwa wagonjwa.

Kuwapa vifaa vya kujikinga kutawawezesha kufanya kazi bila woga wala hofu na kwa kujiamini zaidi, jambo ambalo pia litawapa imani na matumaini wagonjwa wanaokwenda katika vituo vya huduma kupata matibabu ya ugonjwa huo.

Vile vile, tunakubaliana na Kamati ya Bunge kushauri serikali kuwapa motisha madaktari na manesi. Kwa kufanya hivyo, tunaamini kuwa watapata morali zaidi ya kutoa huduma kwa bidii na kwa ufanisi mkubwa.

Mbali na kukubaliana ushauri wabunge kwa serikali, pia tumefarijika na hatua mbalimbali ambazo serikali ilizitangaza jana za kukabiliana na corona.

Hatua hizo ambazo zilitangazwa jana na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alipokuwa akiwasilisha hotuba yake, alisema serikali imetoa mafunzo ya kukabiliana na ugonjwa wa (Covid-19) kwa wataalamu wa afya 2,113 wa mikoa 11 nchini.


Aidha, serikali imeimarisha uwezo wa kupima sampuli kwa watu wote wanaohisiwa kuwa na viashiria au dalili za ugonjwa huu, na kwamba kwa sasa Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii imejengewa uwezo kwa kupatiwa mahitaji yote muhimu katika kupima virusi.

Pia Waziri Ummy alisema serikali imekukamilisha ujenzi na uungaji wa vifaa katika jengo jipya kwa ajili ya kukabiliana na corona. Kadhalika, watumishi 120 wameajiriwa kwa muda ili kuimarisha ufuatiliaji wa wasafiri wanaoingia nchini kupitia maeneo ya mipakani na kwamba serikali imeandaa utaratibu maalum wa kuwaweka chini ya uangalizi wa siku 14 kwa gharama zao.

Kitu muhimu cha kutilia maanani ni kuwa ugonjwa huu ni hatari na haubagui mtu yeyote kwani haujali umri, cheo, elimu, uwezo kiuchumi, rangi, dini wala taifa, hivyo ni jambo la msingi Watanzania wote tukawa kitu kimoja ikiwamo kushauriana na kukubaliana kuhusiana na mbinu na mikakati katika kukabiliana na gonjwa hili.

Ni matarajio kuwa serikali itapokea na kufanyia kazi ushauri huo mzuri wa wabunge wetu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kulikoni wafanyabiashara wagomea sukari bei juu?

Na Sabato Kasika

**SERIKALI** imetangaza bei elekezi ya sukari katika mikoa mbalimbali nchini, ikiwa ni namna ya kupambana na mfumuko wa ghafla wa bei ya bidhaa. Hilo limeibuka hivi karibu na kusababisha sintofahamu kwa walaji.

Baadhi ya wafanyabiashara walipandisha kufikia wastani wa Sh. 4,000 hadi Sh. 4,500 kwa kilo kwa bei ya rejareja, tofauti ilivyokuwa ikiuzwa siku za nyuma ikiwa ni Sh. 2,600 kwa kilo kuwa kiwango cha juu.

Kutokana na sintofahamu, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, aliingilia kati na kisha Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, akaendeleza kwa kutoa bei elekezi kwa mkoa Dar es Salaam, ambayo Sh. 2,600, huku mingine nayo ina bei zake.

Mathalani Sh. 2,900 ni kwa mikoa ya Njombe, Iringa, Simiyu, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Geita, Singida na Dodoma, huku Sh. 2,700 inaangukia Manyara, Pwani, Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Morogoro. Lindi na Mtwara, bei yao kwa kilo moja ya sukari Sh. 2,800, mikoa ya Mbeya, Kagera, Mara na Songwe bei ikiwa ni Sh. 3,000, wakati mikoa ya Rukwa, Kigoma, Katavi na Ruvuma bei yake ni Sh. 3,200.

Hiyo ndiyo bei elekezi iliyotolewa, huku Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, naye anawaonya wafanyabiashara watakaojaribu kupandisha bei za vyakula wakati wa mfungo wa mwezi wa Ramadhani.

Anasema, hadi sasa kuna sukari ya kutosha nchini, hivyo bei itabaki ileile pasipo kujali msimu. Ameshawaagiza wakuu wa mikoa na wasaidizi wao wilayani, kuwachukulia hatua kali za kisheria wafanyabiashara watakaouza sukari kwa kuzidi Sh. 4,500.

Pamoja na serikali kuingilia kati kutangaza bei elekezi, bado wapo baadhi ya wafanyabiashara wasiozingatia maelekezo hayo na badala yake, wanaendelea kuuza bidhaa hiyo kwa bei wanayojua wenyewe.

Nipashe imeshuhudiwa baadhi ya maduka jijini Dar es Salaam, mfano maeneo ya Ukonga na Kinyerezi, ikuza bidhaa hiyo kwa bei kati ya Sh. 3,000 na Sh. 3,200.

Tayari kwa wasiofuata maelekezo wameanza kukamatwa, kwani inaelezwa wafanyabiashara saba wilayani Hai mkoani Kilimanjaro, wametiwa mbaroni baada ya kubainika kupuuza maelekezo ya serikali.

Katika mkoa huo, sukari inatakiwa kuuzwa kwa Sh. 2,700 kwa kilo kwa bei ya rejareja, lakini inaelezwa kuwa baadhi ya wafanyabiashara waliokamatwa walikuwa wakiuza kwa Sh. 3,500 kwa kilo.

Serikali imeshasema kuwa sukari ipo ya kutosha, sasa kwa nini wafanyabiashara wapandishe bei? Wanachotafuta ni nini? Walaji waamini kuwa bidhaa hiyo imeadimika?

Kuna mtazamo kwamba sukari inaweza kufichwa kwa sababu kuu mbili, mosi ni kulazimisha, ili iuzwe kwa bei kubwa inayomletea faida muuzaji, hali yenye athari kwa mlaji.

Pili, inadaiwa huenda wafanyabiashara wanatengeneza uhaba wa makusudi, kuiaminisha serikali kuna uhaba wa bidhaa hiyo nchini, ili wapewe vibali vya kuagiza sukari kutoka nje ya nchi.

Haipendezi kuficha bidhaa na kuchochea mfumuko wa bei pasipo sababu za msingi, hali inayozaa maumivu kwa umma, ambao ni miongoni mwa wateja wa kila siku wa bidhaa hiyo muhimu.

Nakumbuka, ilishawahi kujitokeza mwaka 2016, serikali ikapambana nayo.

Lakini baada ya kutulia kwa kipindi hicho chote, sakata la kupanda bei ya sukari limeibuka tena na kuifanya serikali ilazimike kutangaza bei elekezi, ambayo hata hivyo ni wazi baadhi ya wafanyabiashara hawataki kuifuata.

Serikali inatangaza kuwa sukari ipo, wafanyabiashara nashangaa inakuwaje bado bei inapandishwa? Si vyema kushindana na mtu aliyeshika mpini, wakati wewe umeshika kwenye makali. Ni wazi utakatwa tu.

Ikumbukwe kuwa, mfanyabiashara mtaji wake ni wananchi na ili biashara iendelee anawahitaji sana.

Mfanyabiashara anapobuni mbinu za kuimarisha faida zikiwamo za kuficha sukari ili iwe adimu mtaani, halafu ukifika muda fulani anaitoa na kuuza kwa bei zenye faida kubwa kwake, ni wazi huo unakuwa ni uhuni au ukaidi.

Hivyo ni wakati wa wafanyabiashara wakatafakari jambo hilo kwamba; serikali inasema sukari ipo ya kutosha na imeweka bei elekezi, hao wafanyabiashara wakaidi sasa wanatafuta nini, wanapoamua kupandisha bei zaidi ya maelekezo rasmi?

Binafsi napongeza hatua zozote zitakazochukuliwa dhidi ya wafanyabiashara ambao kwa namna moja au nyingine, wanajaribu kuwaumiza wananchi kwa gharama pasipo na sababu za msingi.

HABARI KITAIFA

# TTB yaja na mkakati kunusuru utalii

**Na Beatrice Philemon**

BODI ya Utalii Tanzania (TTB) imeandaa na kurusha makala fupi ya dakika 1.5 katika masoko yote makubwa ya utalii yaliyopo katika nchi mbalimbali duniani ili kuhamasisha watalii kujikinga na COVID-19 na kuwakumbusha wasifute safari zao za utalii nchini.

Badala yake bodi hiyo imewataka watalii hao waahirishe safari zao hadi wakati mwingine, ambapo dunia itakuwa salama kwa safari.

Hatua hiyo ilitangazwa jana na Mwenyekiti wa TTB, Jaji Thomas Mihayo, alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari kuhusu janga la COVID-19 na utalii wa Tanzania pamoja na hatua zilizochukuliwa na bodi.

"Makala hii fupi imeishazunguka katika masoko yetu yote makubwa ya utalii likiwamo soko la utalii la Marekani, Italia, Hispania, Uingereza, Ujerumani, China na nchi zingine, na imefanikiwa kuvuka matarajio yetu ya awali ya kiwango cha watu waliyoiona," alisema.

Jaji Mihayo alisema kuwa pia balozi za nje zimepatiwa makala hiyo kwa ajili ya kuisambaza kwenye masoko yao.

Alisema kadhalika, makala imeonyeshwa kwenye vituo vya television nchini, na imetafsiriwa na kuwekwa maandishi kwa lugha za Kiarabu, Kifaransa, Kijerumani na Kidachi.

"Vile vile TTB, Hifadhi za Taifa Tanzania (Tanapa) na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) wameingia ubia na kampuini binfasi ya utalii inayojulikana kama "Great Migration Camp" na kubuni kipindi maalum kinachoitwa 'Serengeti Live Show'."

Alisema vipindi vyake vitarushwa mubashara na vingine vitarekodiwa na kurushwa kwa awamu kwenye mitandao ya TTB na washirika wake nchini na nje ya nchi kuonyesha utalii wa Tanzania.

"Madhumuni ya vipindi hivi ni kukonga mioyo ya watalii ambao wameahirisha safari zao Tanzania kwa kipindi hiki cha COVID-19 kupitia televisheni na mitandaoni," alisema Jaji Mihayo.

Akielezea janga la COVID-19, alisema taarifa iliyotolewa Machi 26, mwaka huu na Shirika la Utalii Duniani (UNWTO), imeonesha kuwa idadi ya watalii duniani itashuka kwa kiwango cha kati ya asilimia 20-30 kwa mwaka 2020.

"Kiwango hicho kitasababisha ukosefu wa mapato kiasi cha dola za kimarekani 300 mpaka 450 bilioni duniani," alisema.

Pia kwa mujibu wa utabiri wa awali uliofanywa na shirika lisilo la kiserikali linaloshauri nchi na taasisi za kimataifa linalojulikana kama "Dcode Economic and Financial Consulting" umeonesha kuwa mwenendo wa uchumi duniani umebadilika na utaendelea kubadilika ambapo sekta ya utalii wa anga zilizokuwa zimeshamili kwa sasa ndiyo zitakazokuwa za mwisho kwenye uchangiaji na ukuaji wa uchumi.

"Sekta ya usafiri wa anga ndiyo imeathirika kwa kiasi kikubwa (ya mwisho) ikifuatiwa na utalii kutoka mwisho," alibainisha.

# Corona yaathiri ukusanyaji damu

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

MLIPUKO wa virusi vya corona, umetajwa kushusha kiwango cha damu iliyokuwa ikikusanywa katika hospitali ya rufani ya Mkoa wa Kagera.

Akizungumza na Nipashe mshauri wa Kituo cha Damu Salama katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kagera, Amos Bashweka, alisema kabla ya shule na vyuo kufungwa kituo hicho kilikuwa kikikusanya zaidi ya chupa 400 kwa mwezi, lakini kwa sasa kinakusanya chupa 200.

"Uhaba huu unatokana na wananchi wa mkoa wa Kagera kutokuwa na utamaduni wa kujitolea kuchangia damu katika hospitali, na hii damu tunayokusanya ndiyo inategemewa kuvigawia vituo vingine vya afya na hospitali," alisema.

Bashweka alisema kabla ya shule na vyuo kufungwa, changamoto ya ukusanyaji damu haikuwa kubwa kama sasa, na kutumia fursa hiyo kuwaomba wananchi kubadilika na kujitokeza kwa wingi kujitolea damu, kwa kuwa inapokuwapo damu inayotosheleza mahitaji, inasaidia kuokoa maisha ya wanaohitaji huduma hiyo.

Hata hivyo, alibainisha kuwa kufungwa kwa shule kutokana na tishio la corona kumechangia hali hiyo kwa kuwa kundi la wanafunzi ni muhimu katika ukusanyaji damu.

Kwa mujibu wa Bashweka, asilimia kubwa ya wanafunzi wachangiaji wanakuwa hawana maambukizi ya magonjwa yanayosababisha damu isitumike.

"Damu tunayokusanya tunaipeleka maabara ya kanda iliyoko jijini Mwanza, inapimwa ili kubaini kama ina maambukizi ya magonjwa mbalimbali ikiwamo virusi vya Ukimwi, homa ya ini na kaswende, lengo ni kuhakikisha inapotumika inakuwa salama," alisema Bashweka.

Aliwashukuru baadhi ya wanafunzi na wanachuo wanaoishi katika Manispaa ya Bukoba ambao licha ya shule na vyuo kufungwa, wamekuwa wakifika katika kituo hicho kujitolea kuchangia damu, na kuwaomba kuendelea na moyo huo, kwa kuwa damu wanayojitolea inaokoa maisha ya wananchi wenzao.

# 'Mpemba', wenzake wamwangukia DPP

**Na Hellen Mwango**

WASHITAKIWA katika kesi ya Uhujumu Uchumi inayomkabili mshitakiwa Yusuf Ali, maarufu kama 'Mpemba wa Magufuli' na wenzake, wameiomba mahakama kumshauri Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) kukubali hati za mali zisizohamishika zinazomilikiwa na ndugu zao kama dhamana ya Sh. milioni 90 ili waweze kutoka mahabusu.

Kadhalika wameiomba mahakama kuwasaidia ili waweze kutoka nje kwenda kutafuta fedha za kulipa kama walivyofanya makubaliano na DPP katika makubaliano yao ya kukiri kosa.

Madai hayo waliyatoa jana kwa njia ya Mahakama Mtandao iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, anayesikiliza kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Wakili wa Serikali, Kandide Nansua, alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kutajwa na kwamba kutokana na kujikinga na virusi vya Corona wameshindwa kumwita shahidi.

Hata hivyo, washitakiwa kwa nyakati tofauti waliiomba mahakama kumshauri DPP akubali kuzipokea hati za ndugu zao ili waweze kutoka kwenda kutafuta fedha za kulipa kama mkataba wao wa makubaliano unavyowataka.

Hakimu Simba alisema sheria ya makubaliano ni mpya imeanza kutumika mwaka 2019 kwa kuelekeza makubaliano ni kati ya mshitakiwa na DPP.

Alisema mahakama haihusiki katika makubaliano hayo.

"Mahakama hii itamshauri Wakili wa Serikali Kiongozi wa hapa Kisutu kushughulikia suala hilo limalizike kwa kuwa mhimili huu unafahamu mlundikano wa watu magerezani," alisema Hakimu Simba.

Alisema kesi hiyo itatajwa Mei 13, mwaka huu na washitakiwa wataendelea kukaa mahabusu.

Yusuph na wenzake watano wanakabiliwa na mashitaka manne, ikiwamo kujihusisha na biashara haramu ya meno ya tembo yenye thamani ya Sh. milioni 785.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa katika tarehe tofauti kati ya Januari, 2014 na Oktoba, 2016 katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Iringa na Mtwara, washitakiwa wanadaiwa kujihusisha na mtandao wa ujangili kwa kukusanya na kuuza vipande 50 vya meno ya tembo vyenye thamani ya Dola za Marekani 180,000 sawa na Sh. milioni 392.8 bila kuwa na kibali cha Mkurugenzi wa Wanyamapori.

Katika shitaka la pili inadaiwa kuwa, Oktoba 26, 2016 wakiwa Mbagala Zakhem, walikutwa na vipande 10 vya meno ya tembo vyenye uzito wa kilo 13.85 vikiwa na thamani ya Dola za Marekani 30,000 (Sh. milioni 65.4).

Pia ilidaiwa kuwa Oktoba 27, 2016, wakiwa Tabata Kisukuru washitakiwa walikutwa na vipande vinne vya meno hayo vyenye uzito wa kilo 11.1 vikiwa na thamani ya Dola za Marekani 15,000 (Sh. miliooni 32.7).

Katika shitaka la nne washitakiwa hao walidaiwa kukutwa na vipande 36 vyenye thamani ya Sh. 294.6 milioni bila kuwa na kibali cha Mkurugenzi wa Wanyamapori kosa wanalodaiwa kulifanya Oktoba 29, 2016.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

**ISO 9001:2015 CERTIFIED**

**TAARIFA KWA UMMA**

**MATUMIZI SAHIHI YA NAMBA ZA SIMU**

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inaendelea kuwakumbusha wananchi na wadau wote wa Mawasiliano kuzingatia matumizi sahihi ya namba za mawasiliano ya simu kulingana na matumizi yake kama yalivyo idhinishwa na TCRA kwa kuzingatia mpango wa kitaifa wa namba za mawasiliano ya simu (National Numbering Plan). Ni kosa la kisheria kwa mtu binafsi au taasisi yoyote kutumia namba yoyote kinyume cha matumizi husika hususani kwa kutoa au kupokea taarifa kwa Umma.

Namba kwa ajili ya kuhabarishana kuhusu majanga hapa nchini hutolewa na TCRA kwa Mamlaka husika na sio vinginevyo. Yeyote atakaye kiuka agizo hili atachukuliwa hatua za kisheria.

**Imetolewa na: MKURUGENZI MKUU**

**Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Mawasiliano Towers**
**20 Barabara ya Sam Nujoma**
**S.L.P. 474**
**14414 DAR ES SALAAM TANZANIA**
**30 Aprili 2020**



Mkazi wa Pugu Bombani Dar es Salaam, Paul Makota, akionyesha athari walizozipata baada ya mvua kubwa kunyesha na kusababisha mafuriko katika makazi yao. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Basi laua dereva, lajeruhi abiria

**Na Said Hamdani, LINDI**

MKAZI wa Gongo la Mboto, jijini Dar es Salaam,Yahya Maneno (50), amekufa papo hapo, na abiria wengine watatu wamejeruhiwa na kulazwa, baada ya gari walilokuwa wakisafiria kushindwa kupanda mlima na kupinduka.

Majeruhi hao wamelezwa katika Hospitali ya Sokoine mkoani Lindi, wakiuguza majeraha.

Baadhi ya abiria waliokuwa wakisafiri na basi hilo aina ya Catar yenye namba za usajili T 192 DLD kutoka Dar es Salaam kwenda Lindi, wameeleza kuwa ajali hiyo imetokea Aprili 28, mwaka huu majira ya usiku.

Sufiani Kalala na Elisia Martini waliokuwa wakisafiri na basi hilo kutoka Dar es Salaam kwenda Tarafa ya Milola, Lindi Vijijini, wamesema basi hilo lilikuwa bovu kwani lilikuwa likitengenezwa mara kwa mara njiani.

Wanaeleza kuwa wakiwa wanapandisha Mlima wa Mitwero, basi hilo lilishindwa kumaliza na kuanza kurudi nyuma, huku dereva, Yahaya Abdallah Maneno, akimuagiza kondakta wake aweke gogo bila mafanikio.

Walisema baada ya dereva kuona gari linashika kasi, alimtaka kondakta wake ateremke akaweke gogo ili lisimame, lakini ikashindikana.

Pia, mashuhuda hao,walisema kutokana na kasi kwenye mteremko, dereva aliruka na alipofika chini, basi lilimuangukia na kufa papo hapo, huku baadhi ya abiria wakijeruhiwa na kupoteza viungo vyao vya mwili.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Sokoine, Dk. Muhaji Mohamed, alithibitisha kupokea mwili wa dereva huyo pamoja na abiria wawili wote wanawake wakiwa wameumia mikono ya kulia, kati yao mmoja umekatika kabisa.

Aliwataja ni Fatuma Selemani (19), mkazi wa Mpilipili, Manispaa ya Lindi, ambaye ameumia mkono wa kulia, Dunia Athumani (29), fundi magari wa Yombo Dovya, jijini Dar es Salaam na Elisia Martini (32), mkazi wa Kongowe, jijini Dar es Salaam, ambaye ameumia mkono wa kulia.

"Kuna huyu mmoja aitwae Fatuma Selemani amepoteza kabisa mkono wake wa kulia," Alisema Dk. Mohamed.

Kamanda wa Polisi mkoani Lindi, Stanley Kulyamo, alisema chanzo ni gari kushindwa kupanda Mlima Mitwero, kisha kurudi nyuma na kupinduka.

Alisema basi hilo lililokuwa likitoka Dar es Salaam kwenda Milola, Lindi Vijijini lilikuwa na abiria 17.

"Ninachowasisitiza madereva na wamiliki wa vyombo vya moto kabla ya kuanza safari viwe vimefanyiwa matengenezo ili kuondoa tatizo kama hili," alisisitiza.

# Mabati ya mil. 80/- ujenzi wa maboma

**Na Tiganya Vincent, TABORA**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kaliua katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Machi, imenunua mabati 300 kwa gharama ya Sh. milioni 80 kutoka mapato ya ndani.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Haruna Kasele, alibainisha hayo wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani.

Alisema bati hizo zitagawanywa katika kata zote ambazo zimekamilisha maboma, ununuzi wa mbao na vifaa kwa ajili ya upauaji.

Aidha, alisema wanaendelea na ujenzi wa vyumba sita vya maabara katika shule za sekondari za Kanoge, Kamsekwa, Zugimulole, Silambo, Seleli na Ilege.

Katika hatua nyingine, Kasele alisema Kaliua imeshapokea shilingi bilioni 1 kwa ajili ya mpango wa elimu bila malipo kutoka Serikali Kuu.

Alisema kwa upande wa shule za msingi wamepokea shilingi milioni 683.9 na shule ya sekondari shilingi milioni 399.8.

Kasele aliishukuru serikali kwa kutoa fedha hizo ambazo zimewawezesha wanafunzi kujiunga na shule za msingi na sekondari.

Wakati huo huo, Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua imetoa mikopo ya shilingi milioni 345 kwa vikundi mbalimbali.

Kasele alisema shilingi milioni 133.5 zimetolewa kwa vijana, shilingi milioni 184 kwa wanawake na milioni 27.5 kwa wenye ulemavu.

Alivitaka vikundi ambavyo vimekopeshwa kuhakikisha vinarejesha fedha hizo ili zikopeshe vikundi vingine.

# Brela kuziwezesha h'shauri leseni biashara kielektroniki

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (Brela), umeahidi kuziwezesha halmashauri na majiji nchini vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) ili zitoe leseni za biashara kielektroniki.

Hayo yalisemwa jana, jijini Dar es Salaam na Kaimu Mkuu wa Idara ya Miliki Ubunifu wa Brela, Seka Kasera, wakati akikabidhi vifaa vya Tehama kwa halmashauri ya Wilaya ya Chalinze, mkoa wa Pwani.

Makabidhiano ya vifaa hivyo yalifanyika jana jijini Dar es Salaam na wawakilishi kutoka halmashauri hiyo.

Kasera alisema lengo la Brela ni kuhakikisha wanasambaza vifaa hivyo kwa halmashauri zote nchini ili huduma ya kutoa leseni za biashara kielektoniki ifike kwenye mikoa yote.

Alisema uwapo wa mfumo huo utasaidia kupunguza urasimu, malalamiko, rushwa na muda wa kufuatilia leseni, kwa uwapo wa huduma hii sasa wafanyabiashara hawatazunguka kutoka ofisi moja kwenda nyingine kufuatilia leseni.

Alisema baada ya kupatiwa vifaa hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze, itaanza kutoa leseni za biashara kielektroniki ili kuwapunguzia usumbufu wafanyabiashara.

Akizungumza katika hafla hiyo, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Leseni kutoka Brela, Peter Riwa, alisema Chalinze itakua halmashauri ya tatu katika mpango wa utoaji wa leseni hizo kwa mfumo huo.

"Baada ya makabidhiano haya, Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze itakua ya tatu katika utoaji wa leseni za biashara kielektroniki baada ya Ilala na Mwanza jiji," alisema Riwa.

Pia alivitaja vifaa vya Tehama vilivyotolewa kuwa ni pamoja na kompyuta za mezani tatu, kompyuta mpakato moja, mashine ya kuchapishia moja, simu za mkononi tatu, modemu mbili na tambazo (scanner) moja.

Mwakilishi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze, ambaye ni Ofisa Biashara wa wilaya, Samson Morris, aliishukuru Brela kwa vifaa hivyo na kuahidi kuvitumia kwa malengo yaliyokusudiwa.

"Mfumo huu utasaidia wafanyabiashara wetu wanaotoka sehemu mbalimbali za vijijini na maeneo mengine yasiyofikika kwa urahisi na pia kuokoa fedha kwa sababu sasa haina haja ya kutumia nauli kufuatilia leseni," alisema Morris.

Mfumo wa utoaji leseni za biashara kundi B ulilenga Halmashauri za Jiji la Mwanza, Manispaa za Ilala na Bukoba, Mji wa Mafinga, Wilaya ya Karagwe na Chalinze.

Majaribio yalianza rasmi Oktoba 1, 2019 katika Halmashauri za Jiji la Mwanza, Manispaa ya Ilala na umeonyesha matokeo chanya hadi sasa.

# Mwili wa mwalimu waopolewa mtoni

**Na Neema Hussein,** KATAVI

MWILI wa Gogadi Funu (35), mwalimu wa shule ya msingi wilayani Nkasi mkoani Rukwa, umeopolewa mtoni siku nne baada ya kudaiwa kusombwa na maji ya Mto Kasimba wilayani Mpanda.

Ilidaiwa kuwa kutokana na mvua kubwa iliyonyesha Aprili 25 mwaka huu, mto huo ulijaa maji na daraja la kuvuka katika mto huo kufunikwa na kusababisha mwalimu kusombwa na maji wakati akivuka na mwili wake kupatikana juzi.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Kamanda wa Polisi mkoani Katavi, Benjamin Kuzaga, alisema jana kuwa mwalimu huyo alikuwa likizo kwa mkewe Verediana Gabriel ambaye ni mwalimu wa Shule ya Msingi Mpanda.

"Kwa sasa hivi kama tunavyojua shule zimefungwa kutokana na janga hili la ugonjwa wa corona, ndipo mwalimu huyo aliamua kuja huku Mpanda kwa mke wake," alisema.

Kamanda Kuzaga aliongeza kuwa mwalimu huyo alikutwa na baa hilo la kusombwa na maji ya mto alipokuwa anatoka eneo la Nsemulwa kurejea nyumbani kwake Misengeleni, Kata ya Ilembo.

"Kutokana na mvua kubwa iliyonyesha siku hiyo, alishindwa kuvuka maji yaliyokuwa yakipita juu ya daraja la mto huo," alisema.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Airtel lilikotokea tukio hilo, Justine Lukensa, alidai huenda mwalimu huyo hakujua kuwa daraja limetengeneza mto wa pili, hivyo kipindi anavuka hakulitambua suala hilo.

Baadhi ya wananchi walioshuhudia uopoaji wa mwili huo, walieleza kusikitishwa na mkasa huo kwa kuwa muda mrefu eneo hilo halijawa na matukio ya aina hiyo.



Mmoja wa waumini wa madhehebu ya dini ya Kiislamu akipokea msaada wa futari na daku kutoka kwa kiongozi wa shirika lisilokuwa la kiserikali la The Islamic Foundation mkoani Singida, jana.

# Watoto 830 wanufaika misaada ya Mo Dewji

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Mo Dewji (Mo Dewji Foundation), imetoa msaada wa bidhaa na vyakula kwa watoto 836 kwa ajili ya mfungo wa Ramadhani.

Kwa kushirikiana na asasi isiyo ya kiserikali ya Volunteers in Development (VID), Taasisi ya Mo Dewji jana ilitoa msaada wa vyakula kwa watoto kwa ajili ya mfungo huo ikiwa ni sehemu ya malengo yake kurudisha kwenye jamii kwa kusaidia wenye uhitaji.

Watoto hao wanatoka kwenye kaya maskini katika maeneo ya Dar es Salaam, Mkuranga, Bagamoyo, Pemba, Mwanza, Kondoa, Arusha na Moshi.

Bidhaa zilizotolewa kwa pamoja kwa ajili ya wahitaji ni pamoja na mafuta ya kupikia, unga wa ngano, unga wa sembe, sukari, mchele, maharage na pakiti za tambi.

Ugawaji wa bidhaa hizo kwa watoto hao unasimamiwa na asasi ya Volunteers in Development (VID) ambao ndiyo waratibu na wasimamizi wakuu.

Ilielezwa na wawakilishi wa taasisi hiyo kwamba, taasisi yao inatoa rai kwa kampuni mbalimbali na watu binafsi kuendelea kuwasaidia watu wenye uhitaji hususan katika kipindi hiki ambacho dunia inapambana na mlipuko wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (Covid-19).

# Serikali za mitaa kinara kwa rushwa

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Mwanza, imesema serikali za mitaa zinaongoza kwa kulalamikiwa dhidi ya vitendo vya rushwa.

Kaimu Mkuu wa Takukuru mkoani Mwanza, Daud Ndyamukama, alisema taasisi hiyo imepokea malalamiko 219 katika kipindi cha Januari hadi Machi, mwaka huu.

"Takwimu zinaonyesha kwa vipindi vitatu mfululizo Januari hadi Machi, serikali za mitaa ndizo zinaongoza kwa kulalamikiwa dhidi ya vitendo vya rushwa," alisema Ndyamukama.

Kati ya malalamiko hayo, alisema 47 yanahusu serikali za mitaa, wenyeviti, watendaji wa vijiji, mitaa, vitongoji na kata huku idara ya elimu ikiwa na malalamiko 37 na taasisi za fedha 17.

Aidha, alisema malalamiko mengine yanahusu mahakama (16), polisi (16), ardhi (13), vyama vya ushirika (12), afya (12) na 24 kutoka Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco), ununuzi, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kilimo, bima, nishati, ujenzi na mifuko ya hifadhi ya jamii.

Pia alisema malalamiko mengine 24 ni kutoka katika taasisi za uhamiaji, ulinzi, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf), usafirishaji, asasi za kiraia, ukaguzi, siasa, maliasili, taasisi za dini na sekta binafsi.

Kutokana na malalamiko hayo, Ndyamukama alitoa wito kwa wananchi kuzingatia makatazo ya vitendo vya rushwa hasa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge na madiwani.

# Alia na matumizi mfuko wa jimbo

MBUNGE wa Wingwi (CUF), Juma Kombo Hamad, amesema kumekuwapo na sintofahamu katika matumizi ya fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, akidai wabunge hawashirikishwi katika utekelezaji wa miradi.

Akiuliza swali bungeni jana, Hamad alisema mbunge anaishia kuidhinisha fedha tu kupitia kikao cha mfuko huo.


"Je, serikali inatoa tamko gani juu ya jambo hilo ambapo mbunge ndiye Mwenyekiti wa Mfuko huo?" Alihoji.

Katika majibu yaliyotolewa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) kwa mbunge huyo, ilielezwa kuwa fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo zinasimamiwa kwa kuzingatia Sheria Na. 16 ya Mwaka 2009.

"Kwa kuzingatia Kifungu cha 10(1) cha sheria, mgawo wa fedha hizo unasimamiwa na Kamati ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo yenye wajumbe saba, inayoongozwa na mwenyekiti ambaye ni mbunge wa jimbo husika," ilisema.

Ilibainisha kuwa fedha hizo haziwezi kutumika bila kuidhinishwa na kamati hiyo ambayo kazi yake ni kuandaa vipaumbele vya miradi itakayotekelezwa kwa fedha zilizopokewa.

"Baada ya kamati kukamilisha kazi yake, Ofisa Masuuli anawajibika kusimamia matumizi ya fedha hizo kwa kuzingatia vipaumbele vilivyopitishwa na kamati na kutoa taarifa ya utekelezaji," ilisema.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

# 'Kahawa haina ruzuku ya mbolea'

BUNGE limeelezwa kuwa zao la kahawa halina ruzuku ya mbolea kutokana na serikali kusitisha utoaji wa ruzuku kwa mazao ya kilimo mwaka 2016/17.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Wizara ya Kilimo ilipojibu swali la Mbunge wa Buhigwe (CCM), Albert Ntabaliba.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji sababu za zao hilo kutokuwa na ruzuku ya mbolea kutoka serikalini.

Wizara hiyo ilijibu kuwa ilisitisha utoaji wa ruzuku katika mazao ya kilimo, ikiwamo kahawa tangu mwaka 2016/2017 na kuacha suala hilo kwa wakulima kuagiza na kununua kwa kuzingatia uwezo na uhitaji wa mnufaika kwa bei zilizo sokoni kwa wakati huo.

Ilifafanua kuwa serikali inatambua umuhimu wa mbolea katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, likiwamo zao hilo.

"Utaratibu wa ruzuku ya pembejeo (mbolea na mbegu) ulianza mwaka 2003/4 hadi mwaka 2016/17 ambapo ruzuku hiyo ilikuwa ikitolewa kwa wakulima wa mazao ya mahindi na mpunga tu," ilisema.

Ilieleza kuwa katika kuboresha mfumo wa upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo hususan mbolea kwa wakulima wa mazao yote nchini, serikali ilibadilisha utaratibu wa ruzuku kwa wakulima.

Wizara hiyo ilisema ilianzisha mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja (Fertilizer Bulk Procurement System-FBPS) ulioanza kutumika msimu wa 2017/2018.

"Mfumo huu wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja unalenga kuhakikisha upatikanaji wa mbolea kwa wakati na kwa bei nafuu kwa kuimarisha utaratibu wa usambazaji wa mbolea," ilisema.

Wizara hiyo iliongeza kuwa malengo mengine ya mfumo huo ni pamoja na kukuza mitaji ya wafanyabiashara wadogo na kushiriki katika biashara ya mbolea, kudhibiti bei ya mbolea, kupunguza gharama za uendeshaji na kurahisisha ufuatiliaji.



# Muswada bima ya afya moja wanukia



WIZARA ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imeandaa mapendekezo ya kuanzisha bima ya afya moja na muswada wake utawasilishwa kwenye Bunge la 12.

Kauli hiyo ilitolewa bungeni jana na wizara hiyo ilipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Kiteto Koshuma (pichani).

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji mpango wa serikali kupeleka bungeni sheria ya kuwataka wananchi wote kujiunga na mifuko ya bima ya afya.

Katika majibu yake, wizara hiyo ilisema inaendelea na maandalizi ya utaratibu wa kuhakikisha wananchi wote wanakuwa katika mfumo huo na kuwa na uhakika wa kupata huduma wakati wowote wanapohitaji bila kuwa na kikwazo cha kifedha.

"Katika kutekeleza jambo hili, wizara imeandaa mapendekezo ya kuanzisha Bima ya Afya Moja (Single National Health Insurance) na kuwasilishwa katika ngazi mbalimbali za uamuzi serikalini," ilisema.

Hata hivyo, wizara hiyo ilisema pindi serikali itakaporidhia mapendekezo hayo, suala hilo litawasilishwa bungeni kujadiliwa na kuamuliwa.

"Endapo Bunge litapitisha muswada huo, kutakuwa na ulazima wa wananchi wote kujiunga na bima ya afya, ni matarajio ya wizara kuwa muswada huu utawasilishwa bungeni kwenye Bunge la 12," ilisema.

Wizara hiyo pia ilisema kwa sasa inaendelea kutekeleza mikakati ya kuhamasisha wananchi kujiunga na bima za afya.

Ilitoa rai kwa wabunge kuendelea kuwahimiza wananchi kujiunga na bima za afya zilizopo wakati wakisubiri muswada huo kupitishwa.

Katika hatua nyingine, Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Mary Muro, alihoji lini Hospitali ya Tumbi Kibaha mkoani Pwani itaongezwa mgao wa dawa na wataalamu katika upande wa upasuaji, hasa ikizingatiwa kuwa majeruhi wa ajali za Barabara ya Morogoro wanategemea hospitali hiyo.

Katika majibu yake kwa mbunge huyo, wizara hiyo ilisema imeongeza bajeti kuhakikisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba unakuwapo muda wote katika hospitali ikiwamo Hospitali ya Tumbi.

"Serikali imeongeza zaidi ya mara tisa bajeti ya dawa na vifaa tiba, kutoka Sh. bilioni 31 mwaka 2015/16 hadi Sh. bilioni 200 mwaka 2019/20," ilisema.

Ilisema ongezeko hilo la kibajeti na usimamizi imara wa rasilimali, vimeongeza upatikanaji wa dawa muhimu katika vituo vya kutolea huduma kutoka asilimia 53 kwa 2015/16 hadi kufikia asilimia 94 kwa 2019/20.

"Wizara ya Afya imeboresha huduma ya dharura na upasuaji katika Hospitali ya Tumbi kwa kuongeza idadi ya madaktari bingwa wa upasuaji hadi kufikia madaktari sita," ilisema.

Iliongeza kuwa kwa sasa inategemea madaktari bingwa watatu waliomaliza masomo na kurudi mwaka huu, pamoja na wengine 13 ambao bado wako vyuoni katika hatua mbalimbali za kukamilisha masomo yao.

Ilisema wataalamu hao wanasoma taaluma mbalimbali za kibingwa na ubingwa bobezi zikiwamo zinazohusiana na huduma kwa waathirika wa ajali za barabarani..

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

## HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO, MHE. UMMY A. MWALIMU (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/2021



*Mhe. Ummy Ally Mwalimu* (Mb)
Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto



*Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile* (Mb)
Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto



*Prof. Mabula Daudi Nchembe*
Katibu Mkuu (Idara Kuu Afya)



*Dkt John Kiang'u Jingu*
Katibu Mkuu (Idara Kuu Maendeleo ya Jamii)

# HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII JINSIA WAZEE NA WATOTO

## HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO, MHE. UMMY A. MWALIMU (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/21

**A. UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2019/20 na Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2020/21. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa mwaka 2020/21. Vilevile, Hotuba hii imeainisha mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitano (5) ya Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na **Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Aidha, ninapenda kutumia fursa hii kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kumshukuru kwa dhati **Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake imara na pia kwa dhamira yake, maono yake na uthubutu wake ambao umekuwa dira sahihi katika utendaji wangu na katika kuimarisha utoaji wa huduma za Afya, Ustawi na Maendeleo ya Jamii nchini. Ni dhahiri kuwa katika kipindi cha uongozi wake Watanzania wameshuhudia mageuzi makubwa katika utoaji wa huduma za afya nchini ikiwemo ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya afya katika halmashauri na mikoa yote nchini, kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na huduma za matibabu ya kibingwa na bobezi katika hospitali za rufaa za mikoa, kanda na za ngazi ya Taifa.

3. ***Mheshimiwa Spika***, Kipekee, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa dira na miongozo yake ya kuhakikisha nchi yetu inaendelea kusimama imara katika wakati huu ambapo dunia pamoja na nchi yetu inapitia katika kipindi kigumu cha mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu ujulikanao kwa lugha ya kitaalamu *COVID-19.*

4. ***Mheshimiwa Spika***, ninapenda kutoa shukrani za dhati kwa **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa mstari wa mbele katika jitihada za kuboresha huduma za afya hususan zinazohusu Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto, Lishe, mapambano dhidi ya Kifua Kikuu sambamba na kuhimiza usawa wa jinsia na uwezeshaji wa wanawake katika jamii yetu.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii pia kumshukuru **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri uliowezesha kuleta tija na ufanisi katika utendaji na kuimarisha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Afy na Maendeleo ya Jamii.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuendelea kutekeleza majukumu yako kwa ufanisi mkubwa katika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza Naibu Spika **Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb)** katika utekelezaji wa majukumu yake. Vilevile, nitumie fursa hii kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kusimamia vyema mijadala ndani ya Bunge.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee ninapenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Peter Serukamba (Mb)**, na Makamu wake, **Mheshimiwa Juma Nkamia (Mb)** kwa ushauri na maelekezo waliyoyatoa wakati wa maandalizi ya Bajeti hii. Pia, nitumie fursa hii kuwakaribisha na kuwapongeza **Prof. Mabula Daudi Mchembe** kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Afya na **Prof. Abel Makubi** kwa kuteuliwa kuwa Mganga Mkuu wa Serikali. Pamoja na pongezi hizo, napenda kuwahikikishia kuwa mimi pamoja na watumishi wote wa Wizara tunaahidi kuwapatia ushirikiano katika kutekeleza majukumu yao ili kwa pamoja tushiriki katika kuboresha upatikanaji wa huduma za afya nchini.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa pole kwako, Bunge lako Tukufu, kwa familia na wananchi kwa vifo vya wabunge wao. Vilevile, natoa pole kwa watanzania wote, waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na magonjwa, ajali, majanga pamoja na wahanga wa vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia. Napenda kutumia fursa hii kutoa **pole kwa wagonjwa na majeruhi wa ajali** waliopo hospitalini na majumbani. Namuomba Mwenyezi Mungu awaponye haraka ili waweze kuendelea na ujenzi wa Taifa.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa maelezo ya awali, ninapenda sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2019/20, Mpango na makadirio ya mapato na matumizi pamoja na maombi ya fedha ya kutekeleza vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2020/21.

**B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2019/20 FUNGU 52 NA FUNGU 53**

10. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imeendelea kuzingatia Sera, Mipango Mikakati pamoja na makubaliano ya Kitaifa na Kimataifa yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya nchini, maendeleo ya wanawake na jinsia. Haki, ulinzi na ustawi wa watoto na wazee.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/20, Wizara yangu ilipanga kutekeleza afua mbalimbali zenye lengo la kuboresha utoaji huduma za Afya, Ustawi na Maendeleo ya Jamii nchini. Naomba kutambua maeneo yafuatayo;

**Mapato na Matumizi ya Fedha Fungu 52 (Idara Kuu ya Afya)**

12. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/20 Wizara na Taasisi zilizo chini yake ilikadiria kukusanya kiasi cha **shilingi bilioni 368.5** kutoka vyanzo vya ndani vya makao makuu ya Wizara, hospitali za Rufaa za Mikoa na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Hadi kufikia Machi 2020, jumla ya **shilingi bilioni 262.4** zilikuwa zimekusanywa, sawa na **asilimia 71.2**.

13. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/20 Wizara kupitia Fungu 52 iliandaa bajeti ya jumla ya **shilingi bilioni 959.1** na kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kati ya fedha hizo kiasi cha **shilingi 415,014,262,000** ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida. Fedha zilizopitishwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ni **shilingi 544,137,902,597**.

14. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Machi 2020, Wizara ilipokea jumla ya **shilingi 391,732,923,520** ya bajeti iliyoidhinishwa. Fedha zilizopokelewa kwa ajili ya **matumizi ya kawaida** katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020 ni **shilingi 302,946,918,091** sawa na asilimia 73 ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mwaka.

15. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa miradi ya maendeleo kiasi cha **shilingi 88,786,005,429** kilipokelewa. Aidha, Wizara kupitia miradi msonge ilipokea dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya **shilingi 216,000,000,000.** Vilevile, Wizara ilipokea kiasi cha **shilingi bilioni 86.2 kutoka Mfuko wa Afya wa Pamoja** ambapo kiasi cha **shilingi bilioni 68.3** kilipelekwa moja kwa moja OR – TAMISEMI kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji na utoaji wa huduma za afya katika ngazi msingi.

**Mapato na Matumizi ya Fedha – Fungu 53 (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii)**

16. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/20, Wizara kupitia Fungu 53, ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi **4,763,596,000** kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia Machi 2020, Wizara pamoja na Taasisi zake imefanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi **2,574,658,966.61 sawa na asilimia 54** ya makadirio ya mapato.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/20, Wizara (Fungu 53) iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu matumizi ya shilingi 31,537,431,013. Kati ya fedha hizo, shilingi **28,777,370,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **2,760,061,013** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi 2020, Wizara imepokea jumla ya shilingi **22,364,375,125** sawa na asilimia 71 ya bajeti kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo.

**C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU CHINI YA IDARA KUU YA AFYA**

**HUDUMA ZA KINGA**

**Chanjo**

19. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia **Mpango wa Taifa wa Chanjo** iliweza kutoa huduma za chanjo kwa watoto wenye umri wa chini ya mwaka mmoja kwa kiwango cha **asilimia 99, ukilinganisha na asilimia 97 mwaka 2015/16** wakati Serikali ya Awamu ya Tano inaingia madarakani. Kutokana na kuimarika kwa huduma za chanjo za watoto nchini, kumechangia **kupungua kwa vifo vya watoto wa umri chini ya mwaka mmoja** kutoka vifo **43 kati ya vizazi hai 1,000 mwaka 2015/16 hadi vifo 9** kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2019/20. Vifo vya **watoto wa umri wa chini ya miaka mitano vimepungua** kutoka vifo 67 kati ya Vizazi hai 1,000 mwaka 2015/16 hadi vifo 11 kati ya vizazi hai 1,000 mwaka 2019/20. Hii ni kulingana na takwimu zinazokusanywa na Wizara kutoka katika vituo vya kutolea huduma za afya

**Afya na Usafi wa Mazingira**

20. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Wizara iliendelea kutekeleza afua na mikakati mbalimbali yenye lengo la kuimarisha hali ya usafi wa mazingira ikiwemo kuendesha Kampeni ya Taifa ya Usafi wa Mazingira yenye kaulimbiu isemayo **USICHUKULIE POA NYUMBA NI CHOO** yenye lengo la kuhimiza **ujenzi na matumizi ya vyoo bora** ambapo mikoa 16 kati ya 26 imefikiwa.

21. ***Mheshimiwa Spika***, hali ya usafi wa mazingira kwa ujumla inaonesha kwamba; **kaya zenye vyoo bora nchini** hadi kufikia Machi 2020 ni **asilimia 62.8** kutoka **asilimia 39.4** mwaka 2015/16 na kaya ambazo **hazina vyoo kabisa** zimepungua kutoka **asilimia 6.1** mwaka 2015/16 hadi kufikia **asilimia 1.8** Machi 2020.

**Huduma ya Lishe Nchini**

22. ***Mheshimiwa Spika***, Lishe bora ni muhimu kwa uhai, ukuaji na maendeleo ya binadamu kiakili na kimwili na hivyo kuchangia katika kuongeza tija katika uzalishaji mali kwa kaya na kuimarisha uchumi wa Taifa kwa ujumla. Afua za Lishe zilizotekelezwa katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020 ni pamoja na: kuimarisha afya na **lishe ya watoto wadogo** kwa kuendesha zoezi la Kitaifa la utoaji wa matone ya Vitamini A ambapo watoto **milioni 8.5 walifikiwa;** na kutoa dawa za kutibu maambukizi ya minyoo kwa watoto walio chini ya miaka mitano - watoto milioni 7.5m. Kutokana na juhudi na mikakati mbalimbali iliyotekelezwa, hali ya lishe nchini imeendelea kuboreshwa ambapo kwa mujibu wa **Utafiti wa Lishe uliofanyika mwaka 2018, hali ya udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano imepungua kutoka asilimia 34.4 mwaka 2015/16 hadi kufikia asilimia 31.8.**

**Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto**

23. ***Mheshimiwa Spika***, tumeendelea kutekeleza kazi mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha huduma **kabla ya Ujauzito**, **huduma wakati wa ujauzito (Antenatal Care) na huduma wakati wa kujifungua.** Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kununua na kusambaza dawa za uzazi salama, kununua vifaa tiba kwa ajili ya Vituo vya afya, mafunzo kwa watumishi na kuwezesha ukarabati wa Vituo vya Afya katika halmashauri mbalimbali nchini.

Matokeo chanya yanaonekana kwa kuangalia Viashiria vikuu vya afya ya uzazi, mama na mtoto ikiwemo:-

i. Wajawazito 1,744,668 walihudhuria kliniki wakati wa ujauzito, ambapo wajawazito 1,343,228 **walitimiza mahudhurio manne au zaidi (ANC4+) sawa na asilimia 77 ikilinganishwa na asilimia 41** kwa mwaka 2015/2016 wakati serikali ya awamu ya tano ikiingia madarakani;
ii. Idadi ya akinamama wanaojifungulia katika vituo vya kutolea huduma imeendelea kuongezeka hadi kufikia **asilimia 83 mwezi Machi 2020 ikilinganishwa na asilimia 64 kwa kip**indi kama hicho mwaka 2015/16; na
iii. Vifo vya watoto wachanga vimepungua kutoka vifo 25 kati ya vizazi hani 1,000 mwaka 2015 hadi kufikia vifo 7 kati ya vizazi hai 1,000 mwaka 2019/20.

**Udhibiti wa UKIMWI**

24. ***Mheshimiwa Spika***, Huduma za **Ushauri Nasaha, Upimaji wa VVU** na Utoaji wa ARVs zimeendelea kutolewa kwa wananchi wote bila malipo mijini na vijijini. Idadi ya watu wanaopima afya zao ili kutambua hali zao za maambukizi ya VVU imekuwa ikiongezeka kila mwaka kutoka jumla ya **watu 6,800,000** mwaka 2015 hadi kufikia **watu 12,392,268** Desemba 2019. Ongezeko hili limetokana na mikakati iliyowekwa na Wizara ya kuhakikisha watu wengi zaidi hasa wanaume wanajitokeza kupima VVU. Aidha, vituo vya kutolea huduma za ushauri nasaha na upimaji wa VVU vimeongezeka kutoka vituo 5,600 mwaka 2015 hadi vituo 6,397 Desemba 2019. **Utekelezaji wa afua hizi umewezesha nchi yetu kupiga hatua katika kufiikia malengo ya kidunia ya Tisini tatu ili kutokomeza UKIMWI**.

**90 ya kwanza** – idadi ya watu wanaotambua hali zao kuhusu VVU imeongezeka kutoka watu 816,408 mwaka 2015 hadi 1,289,125. Hii ni sawa na asilimia 58.3 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 80.6 mwezi Desemba 2019.

**90 ya pili –** takwimu pia zinaonyesha watu 1,271,666 sawa na asilimia 98.6 walianza kutumia dawa za kufubaza makali ya virusi vya UKIMWI kulinganisha na watu 740,745 (asilimia 91) walioanzishwa dawa za ARVs mwaka 2015.

**90 ya tatu –** asilimia 98.6 ya watu wanatumia ARVs wamefanikiwa kupunguza wingi wa VVU mwilini kulinganisha na asilimia 83 mwaka 2015.

**Udhibiti wa Kifua Kikuu na Ukoma**

25. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imefanikiwa kuongeza kasi ya ugunduzi wa wagonjwa wa Kifua Kikuu ambapo **kiwango cha ugunduzi wa wagonjwa wa Kifua Kikuu kilipanda hadi kufikia asilimia 53 Machi mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 40 mwaka 2016**. Wagonjwa waliogundulika kuwa na Kifua Kikuu wamepatiwa matibabu ambapo asilimia 91 ya wagojwa waliopewa matibabu wamepona Kifua kikuu kabisa na kuendelea na shughuli zao za ujenzi wa Taifa. **Vifo vitokanavyo na ugonjwa wa Kifua**

# HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII JINSIA WAZEE NA WATOTO

**Kikuu kwa mwaka vimepungua kutoka vifo 30,000 mwaka 2015/16 hadi kufikia 22,000 mwaka 2020.**

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa **huduma za Ukoma**, kaya 131 zimetembelewa (contact tracing) na kufanya uchunguzi wa Ukoma katika wilaya 7 za Muheza, Mkinga, Chato, Ifakara, Kilombero, Nanyumbu na Liwale. Hadi kufikia Machi, 2020 idadi ya wagonjwa waliokuwa wamegunduliwa ilikuwa 1,151 nchi nzima ikilinganishwa na wagonjwa 2,297 kwa kipindi kama hiki cha mwaka 2015/16. Vilevile, **idadi ya watoto wanaougua Ukoma imepungua kwa asilimia 54, kutoka watoto 98 mwaka 2015/16, hadi kufikia watoto 53 Desemba, 2019.**

**Udhibiti wa Malaria**

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo imeendelea kuhakikisha kuwa, dawa za kutibu malaria na vitendanishi zinapatikana wakati wote kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya. Wizara tumegawa jumla ya vyandarua vyenye dawa bila malipo **3,212,748** ambapo vyandarua 1,951,689 viligawiwa kwa wajawazito; na vyandarua 1,261,059 kupitia wanafunzi wa shule za msingi. Aidha Wizara imefanya Uhamasishaji wa jamii kupitia kampeni mbalimbali ikiwemo "**sio kila homa ni malaria", "Zero malaria inaanza na mimi"** na hivyo nchi yetu kupata mafanikio makubwa katika mapambano dhidi ya malaria. **Maambukizi ya Malaria yamepungua kutoka asilimia 14.8 mwaka 2015/16 hadi kufikia asilimia 7.3 Machi 2020. Aidha, vifo vitokanavyo na malaria vimepungua kutoka vifo 6,311 mwaka 2015 hadi kufikia vifo 2,079 Machi 2020.**

**Udhibiti wa Magonjwa ya Mlipuko**

**28.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha utayari wa kukabiliana na tishio la mlipuko wa Ugonjwa wa **Ebola; Ugonjwa ya Homa Kali ya Mapafu (COVID-19);** na **Homa ya Manjano** Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kudhibiti magonjwa haya. Katika kudhibiti kuingia kwa ugonjwa wa **Ebola** nchini, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za kinga katika maeneo ya mipakani kwa kuwajengea wataalam uwezo wa kudhibiti na kukabiliana na ugonjwa huu endapo utaingia nchini. Mwezi Desemba 2019, kulitokea ugonjwa wa mlipuko ulioanzia katika Jimbo la Wuhan nchini China uliojulikana kama **Corona Virus Disease 2019 (COVID-19),** Ugonjwa huu hauna tiba wala kinga, na unasababishwa na kirusi kipya aina ya *Novel Corona* ambacho huathiri zaidi mfumo wa upumuaji wa muathirika na huweza hata kusababisha kifo kama mgonjwa hatapatiwa uangalizi wa uhakika. Shirika la Afya Duniani liliutangaza rasmi ugonjwa huu wa COVID-19, kuwa ni Dharura ya Jamii Kimataifa (*Public Health Emergency of International Concern)* tarehe 30 Januari 2020 na tarehe 11 Machi, Shirika la Afya Duniani (WHO) lilitangaza ugonjwa huu kuwa ni Janga la Dunia *(Pandemic)*.

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania ni mojawapo ya nchi zilizoathirika na janga hilo, ambapo hadi tarehe 24 Aprili, 2020 jumla ya **wagonjwa 284** walithibitika kuwa na maambukizi ya COVID-19 nchini. Kati yao waliopona ni 48 na waliofariki ni ni 10, wagonjwa wengine wote waliobakia (226) isipokuwa 7 hali zao ni nzuri na wanaendelea na matibabu katika sehemu walizotengwa. *Napenda kuwashukuru watumishi wote wa Afya nchini hususani walio mstari wa mbele kwa kujitoa na kufanya kazi bila kuchoka katika kukabiliana na ugonjwa huu tokea ulipoingia nchini. Serikali itaendelea kutambua na kuthamini mchango wao katika kuhudumia wagonjwa na kuokoa maisha. Nasi tutaendelea kutimiza wajibu wetu kwa kuhakikisha uwepo wa vifaa kinga na vifaa tiba katika utoaji wa huduma kwa wananchi.*

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** *aidha, nachukua fursa hii kuwashukuru wananchi kwa kuzingatia maelekezo mbalimbali tunayowapatia ikiwemo kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka. Tunaendelea kuwakumbusha watanzania kuwa ugonjwa huu ni wa hatari na hauna kinga wala tiba, na njia pekee ya kujikinga na ugonjwa huu ni kufuata maelekezo ambayo yamekuwa yakitolewa na wataalam kuhusu namna bora za kujikinga na ugonjwa huu wa corona. Nitumie fursa hii pia kumshukuru Mhe Rais, kwa maelekezo yake ya mara kwa mara katika kudhibiti ugonjwa huu. Kipekee ninamshukuru Mhe. Waziri Mkuu kwa ushirikiano mzuri walionipatia katika kipindi hiki. Aidha, tunawashukuru Wadau wa ndani na nje ya nchi wanaoendelea kuunga mkono jitihada za Serikali za kudhibiti ugonjwa huu nchini.*

**HUDUMA ZA TIBA**

**31.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za tiba nchini kwa kutekeleza majukumu mbalimbali na kuweza kupata mafanikio makubwa. Pamoja na mafanikio mengi yaliyopatikana naomba nitambue yafuatayo:-

**Uimarishaji wa huduma za Matibabu ya Kibingwa na Kibingwa Bobezi nchini**

**32.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020 Wizara kupitia hospitali ngazi ya Taifa na kanda imepunguza Rufaa za wagonjwa nje ya nchi kufikia **wagonjwa 92 waliokuwa na mahitaji ya kupatiwa matibabu nje ya nchi ikilinganishwa na rufaa 554 mwaka 2015/16.** Hali hii inatokana na kutekelezwa kwa afua mbalimbali zilizolenga kujenga uweza wa Hospital iza hapa nchini ili ziweze kutoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi.

Huduma hizi za kibingwa na kibingwa bobezi zimeendelea kutolewa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Mloganzila, Tasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Hospitali ya Benjamin Mkapa – Dodoma, Hospitali ya Afya ya Akili Mirembe, Hospitali ya Kibong'oto, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya, Hospitali ya kanda ya Ziwa Bugando na Hospitali ya kanda ya Kaskazini – KCMC. Pamoja na Huduma za kibingwa na kibingwa bobezi naomba nitambue huduma zifuatavyo:-

i. Huduma ya **upandikizaji wa figo** ambapo jumla ya wagonjwa 18 walipata huduma hiyo;
ii. Huduma ya **upandikizaji vifaa vya usikivu** kwa watoto 9 ulifanyika;
iii. Huduma ya **interventional radiology** ilifanyika kwa wagonjwa 288 ili kuruhusu upasuaji wa shingo na kichwa, kuondoa uvimbe kwenye sehemu ya kinywa, uso na shingo, kuweka mirija kwenye figo, kuzibua mirija ya nyongo iliyoziba, kuzibua mirija ya uzazi na kuondoa usaha ndani ya tumbo;
iv. Huduma za kubadilisha nyonga 145; goti 159; upasuaji wa goti kwa kutumia matundu 198; upasuaji wa mfupa wa kiuno 46; upasuaji wa uti wa mgongo 330; ubongo 139; watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi 284; upasuaji wa mfupa wa paja (femur) 266 ulifanyika;
v. Huduma ya **uchunguzi na tiba za nyuklia kwa ugonjwa** wa Saratani zilitolewa kwa wagonjwa 1,831; na
vi. Huduma za **upasuaji wa moyo bila kufungua kifua** kwa kutumia mtambo maalum *Catheterization Laboratory* ulifanyika kwa wagonjwa 1,551.

**Hospitali za Rufaa za Mikoa**

**33.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Hospitali 28 za Rufaa za Mikoa zilihudumia jumla ya wagonjwa 2,532,650 ikilinganishwa na wagonjwa 3,292,103 waliohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19.

**34.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha utoaji wa huduma za afya, Wizara inatekeleza mradi wa **ujenzi wa Miundombinu ya kutolea huduma za afya katika** hospitali za Mikoa ya; **Njombe** (Jengo la maabara, jengo la huduma za Uzazi na Mtoto, jengo la Upasuaji, jengo la huduma za dharura, jengo Benki ya damu, jengo la kufulia nguo), **Simiyu** (Jengo la maabara, jengo la huduma za Uzazi na Mtoto, jengo la Upasuaji na Radiolojia), **Geita** (Jengo la maabara na jengo la huduma za Uzazi na Mtoto), **Katavi** (Jengo la kutoa huduma za wazazi, dharura, wagonjwa wa nje, famasia, radiolojia, na wagonjwa mahututi), **Songwe** (jengo la wagonjwa wa nje, jengo la maabara na jengo la huduma za afya ya uzazi na mtoto), **Mara –** Mwalimu Nyerere Memorial Hospital, (jengo moja linalotoa huduma za utawala, wagonjwa wa nje, wagonjwa wa ndani, uchunguzi wa magonjwa, famasia, utakasaji wa vifaa, dharura, upasuaji na mahututi).

Miradi mingine ya miundombinu inaendelea kutekelezwa katika mikoa ya; **Dar es Salaam - Mwananyamala** (jengo la huduma za afya ya uzazi na mtoto), **Mwanza** (jengo la kutolea huduma za afya ya uzazi na mtoto), **Kilimanjaro** (jengo la kutolea huduma za afya ya uzazi na mtoto), **Kigoma** (jengo la upasuaji), **Tabora** (jengo la kutolea huduma za dharura), **Iringa** (jengo la kutolea huduma za dharura), **Mbeya** (jengo la kutolea huduma za dharura, wodi ya upasuaji, jengo la huduma za upasuaji na utakasaji wa vifaa), **Ruvuma** (jengo la kutolea huduma za dharura), **Rukwa** (jengo la kutolea huduma za dharura), **Kagera** (jengo la kujifungulia na jengo la upasuaji), **Shinyanga** (jengo la huduma ya afya ya uzazi na mtoto), **Manyara** (jengo la wagonjwa wa nje na jengo la utawala), na **Singida** (jengo la kutolea huduma za maabara, famasia, upasuaji na wodi za wagonjwa).

**UGHARAMIAJI WA HUDUMA ZA AFYA**

**35.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea na jitihada za kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya kuboresha huduma za afya nchini kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo ikiwemo **Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund),** ambapo kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, kiasi cha Shilingi 86,222,819,841 kimepokelewa kupitia Mfuko huo ikilinganishwa na Shilingi 92,440,912,680 zilizopokelewa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi 68,313,229,142 sawa na asilimia 79.2 ya fedha zote zilizopokelewa zilipelekwa na kutumika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa lengo la kuboresha huduma za afya ngazi ya msingi.

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020 Wizara ilipokea jumla ya Shilingi 25,867,451,925.22 kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kutekeleza afua mbalimbali katika sekta ya Afya

**37.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inaendelea na maandalizi ya kutunga sheria ya bima ya afya kwa watu wote. Kwa hivi sasa Serikali ipo katika hatua za mwisho ikiwa ni pamoja na kukusanya maoni ya wadau kwa kabla ya kuanza kuandaa Muswada wa sheria hiyo.

**RASILIMALI WATU KATIKA SEKTA YA AFYA**

**38.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ilifanya **udahili wa wanafunzi 25,077** sawa na asilimia 57.2 ya wanafunzi 43,835 waliotuma maombi kujiunga na vyuo vya Afya. Kati yao wanafunzi 5,682 sawa na asilimia 22.7 walichaguliwa kwenye vyuo vya Serikali vya afya na wanafunzi 19,395 sawa na asilimia 77.3 walichaguliwa kwenye vyuo binafsi na taasisi za dini katika program za Uuguzi na Ukunga na Sayansi Shirikishi za Afya.

**39.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kushughulikia suala la **ajira za watumishi katika Sekta ya Afya,** Wizara imeendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, jumla ya wataalam 1,817 wa kada mbalimbali waliajiriwa na kupangiwa katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya nchini. Aidha, Wizara imetangaza nafasi 1,000 za madaktari ambazo zilitolewa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Februari 2020, wakati akizungumza na Madaktari kupitia Chama cha Madaktari Tanzania (MAT).

**MABARAZA YA WANATAALUMA NA BODI ZA USHAURI ZA AFYA**

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la **kusimamia utendaji wa wataalam wa Sekta ya Afya.** Katika kutekeleza hilo, mabaraza na bodi mbalimbali za kitaaluma ziliundwa kisheria kwa ajili ya kusimamia majukumu hayo. Mabaraza na bodi za kitaaluma ni pamoja na; Baraza la Madaktari Tanganyika, Baraza la Afya Mazingira, Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala, Baraza la Uuguzi na Ukunga, Baraza la Famasia, Baraza la Wataalam wa Macho, Baraza la Radiologia, Baraza la Wataalam wa Maabara, Bodi ya Maabara Binafsi za Afya (PHLB) na Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi. Utekelezaji wa majukumu ya Mabaraza na Bodi hizi katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 umewezesha uwepo wa ufanisi wa utoaji wa huduma kwa wataalam wa afya pamoja na vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

**D. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI CHINI YA IDARA KUU YA AFYA (FUNGU 52)**

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu imeendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Mfuko wa Bima ya Taifa (NHIF), Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Kwa kifupi naomba nitambue yafuatayo:-

i. **Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya** umesajili jumla ya wanachama wapya 364,007 na hivyo kuwezesha Mfuko kuwa na jumla ya wanufaika 4,858,022 sawa na asilimia 9 ya Watanzania wote, ikilinganishwa na wanufaika 3,377,023 mwaka 2015/16;

ii. Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya umesajili jumla vituo vipya 384 vya kutolea huduma za afya nchini vilisajiliwa na kuanza kutoa huduma na hivyo kufikia vituo 7,940 ikilinganishwa na vituo 6,439 vilivyokuwa vimesajiliwa mwaka 2015/16;

iii. **Mamlaka ya Dawa na VifaaTiba (TMDA)** ilifanya tathmini ya maombi 837 ya usajili wa dawa za binadamu kati ya 942 yaliyokuwepo katika kipindi husika. Maombi 572 kati ya maombi yaliyofanyiwa tathmini yaliidhinishwa na hivyo kusajiliwa;

iv. Mamlaka ya Chakula na Dawa ilipokea Maombi 340 ya usajili wa vifaa tiba na vitendanishi ambapo maombi 270 yalifanyiwa tathimini na kati ya hayo 106 yalikidhi vigezo vya usajili;

v. **Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA)** ilipokea jumla ya sampuli 52,917 kwa ajili ya uchunguzi wa Kimaabara unaojumuisha maswala ya kijinai na kijamii, maji, maji taka, kemikali, vyakula, dawa na bidhaa nyingine za viwandani. Sampuli zilizochunguzwa ni 52,249 sawa na asilimia 98.7;

vi. Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imepokea na kuitikia wito wa mahakama kwenye jumla ya kesi 1,278 kwa lengo la kutoa ushahidi wa kitaalam (expert opinion) na ambao umeisaidia vyombo mbalimbali vya kimaamuzi kutekeleza majukumu yao kwa wakati; na

vii. **Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR)** iliendelea kutekeleza tafiti mbalimbali ikiwa ni pamoja na: Utafiti wa Tiba ya Tahadhari ya MALARIA kwa Wajawazito; Utafiti wa KIFUA KIKUU unafualitilia mwenendo wa ugonjwa wa Kifua Kikuu na viashiria vya madhara ya muda mrefu ya kifua kikuu cha mapafu na athari zake kwa afya ya umma (TB Sequel project); Utafiti wa EXIT TB.

**E. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU CHINI YA IDARA KUU YA MAENDELEO YA JAMII (FUNGU 53)**

**Ushiriki wa Jamii katika Shughuli za Maendeleo**

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu dhana ya **ushirikishaji wananchi katika shughuli za maendeleo** ili kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kutumia nguvukazi pamoja na rasilimali zinazowazunguka katika maeneo yao. Mfano ujenzi wa vyumba vya madarasa, ujenzi wa madaraja ya gharama nafuu kwa kutumia teknolojia rahisi na Ujenzi wa Zahanati.

**43.** ***Mheshimiwa Spika***, kupitia **kampeni ya ujenzi wa nyumba bora,** wananchi wamehamasishwa kujenga nyumba bora 751

# HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII JINSIA WAZEE NA WATOTO

katika mikoa ya **Pwani, Katavi, Singida** na **Mwanza**. Ujenzi wa nyumba bora moja unagharimu kiasi cha **shilingi 9,500,000 hadi shilingi 12,579,330** kwa nyumba yenye vyumba vitatu, sebule, choo na jiko kwa kutegemea aina ya ujenzi katika eneo husika. *Nitumie Bunge lako tukufu kuwashukuru na kuwapongeza wananchi kwa kujitolea katika kutekeleza miradi ya maendeleo. Ni matumaini yangu kuwa, wataendelea kujitokeza kutekeleza miradi mbalimbali ya jamii na mtu mmoja mmoja katika maeneo yao. Serikali itaendelea kutambua na kuthamini mchango wa wananchi katika kutekeleza miradi ya maendeleo.*

**Mafunzo ya Taaluma ya Maendeleo ya Jamii**

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia utoaji wa **mafunzo kwa kada ya Maendeleo ya Jamii kupitia Vyuo 8 vya Maendeleo ya Jamii**. Katika mwaka 2019/20, jumla ya **wanafunzi 3,986 walidahiliwa** ikilinganishwa na **wanafunzi 2,015 waliodahiliwa mwaka 2015/16.**

**Haki na Maendeleo ya Mtoto**

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea **kuratibu na kusimamia utoaji wa haki za mtoto** zikiwemo **haki ya kuishi, kulindwa, kuendelezwa, kushiriki na kutobaguliwa**. Hadi kufikia Machi 2020, Wizara imewezesha uanzishwaji wa **Madawati 10 ya Jinsia na Watoto katika vituo vya Polisi**. Idadi ya madawati imeongezeka kutoka madawati 417 mwaka 2015/16 na kufikia madawati 427 Machi, 2020. Uwepo wa Madawati haya umewezesha kuongezeka kwa utoaji wa taarifa za matukio ya ukatili dhidi ya watoto kutoka matukio 10,551 mwaka 2016 hadi kufikia matukio 15,680 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 49.

**Huduma kwa Watoto walio katika Mazingira Hatarishi**

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** huduma za msingi za malazi, chakula, malezi, mavazi, ulinzi, matibabu na elimu zimeendelea kutolewa kwa watoto walio katika mazingira hatarishi wanaoishi katika makao ya watoto nchini. Katika mwaka 2019/20, watoto 75 walipatiwa huduma za msingi kwenye Makao ya Taifa ya Watoto Kurasini yanayomilikiwa na Serikali mwaka 2019/20 ikilinganishwa na watoto 71 waliopata huduma mwaka 2018/19. Idadi ya watoto wanaopata huduma katika Makao ya Watoto imeongezeka kutoka watoto 4,379 mwaka 2015/16 hadi kufikia watoto 15,365 Machi, 2020. *Nitumie fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kutoa wito kwa jamii kuzingatia misingi na utamaduni wa kitanzania wa kuwajibika kutoa malezi, matunzo na ulinzi kwa watoto, ili kuepusha watoto kulelewa katika Makao ya Watoto.*

**47.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, **imewatambua jumla ya watoto 2,398,354 walio katika mazingira hatarishi wakiwemo watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani**. Watoto hawa wamepatiwa huduma mbalimbali ikiwemo chakula, malazi, mavazi, matibabu, vifaa vya shule, ada, ujuzi na huduma za msaada wa kisaikolojia na kuwaunganisha na familia zao. *Kupitia Bunge lako Tukufu napenda kutoa wito kwa Halmashauri zote kuwatambua watoto, kutafuta familia zao na kuwaunganisha na familia zao.*

**Usuluhishi wa Migogoro ya Ndoa na Matunzo ya Watoto**

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea **kufanyia kazi mashauri ya migogoro ya ndoa katika jamii kupitia Mabaraza ya Usuluhishi ya Ndoa.** Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, mashauri ya migogoro ya ndoa 38,659 yalipokelewa na kufanyiwa kazi. Kati ya mashauri hayo, mashauri 3,464 yalifikishwa mahakamani, mashauri 19,272 yamesuluhishwa na mashauri 15,923 yanaendelea kufanyiwa kazi.

**Huduma za Ustawi wa Jamii kwa Wazee**

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea **kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003** ili kuhakikisha ulinzi na usalama kwa wazee. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, **mabaraza ya wazee 2,292 yameanzishwa** katika ngazi mbalimbali hadi kufikia mabaraza ya wazee 14,425. Mabaraza haya hutumika kama majukwaa ya wazee kujadili masuala yanayohusu haki zao.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia imeendelea kuwawezesha wazee kupata huduma za matibabu bila malipo ili kuboresha afya zao. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, jumla ya wazee 167,566 wamepata vitambulisho vya matibabu bila malipo. Hatua hii imewezesha wazee waliopata vitambulisho vya matibabu bila malipo kuongezeka kutoka wazee 213,025 mwaka 2015/16 hadi kufikia wazee 856,052 Machi 2020, sawa na ongezeko la asilimia 301.

**Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi**

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kutekeleza programu mbalimbali za kuwawezesha wanawake kiuchumi. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari 2020, Serikali kupitia utengaji wa **asilimia 4** ya mapato ya ndani ya Halmashauri imetoa mikopo yenye masharti nafuu kiasi cha **shilingi bilioni 12.92** kwa vikundi 8,207 vya wanawake. Kiasi cha mikopo kilichotolewa kimeongezeka kutoka **shilingi bilioni 3.39** zilizotolewa kwa vikundi 2,225 vya wanawake mwaka 2015/16 hadi **shilingi bilioni 52.92** zilizotolewa kwa vikundi 28,230 vya wanawake hadi kufikia Machi, 2020. Aidha, Serikali kupitia **Dirisha la Wanawake** lililoanzishwa katika Benki ya Posta Tanzania (TPB) imeendelea kutoa mikopo kwa wanawake wajasiriamali kwa riba ya **asilimia 3** kwa mwezi. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, mikopo yenye thamani ya **shilingi 3,586,400,000** imetolewa kwa **wanawake wajasiriamali 14,271** ikilinganishwa na kiasi cha **shilingi 2,050,100,000** kilichotolewa kwa **wanawake wajasiriamali 3,035** mwaka 2018/19, sawa na ongezeko la asilimia 75.

**Kuzuia Ukatili wa Kijinsia**

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea na jitihada za kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa kutekeleza kampeni ya **"Tokomeza Ukatili, Twende Pamoja"** kupitia Misafara ya Kijinsia (Gender Caravans). Katika Mikoa ya Katavi, Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa, Tabora, Shinyanga, Simiyu Arusha, Manyara, Singida, Mwanza. Lengo la misafara hii lilikuwa ni kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara ya ukatili wa kijinsia ambapo jumla ya wananchi 9,000 walipatiwa elimu hiyo.

**Kuimarisha Usawa wa Jinsia na Haki za Wanawake**

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia imeendelea kuratibu uingizaji wa masuala ya jinsia katika sera, mikakati na miongozo mbalimbali. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, Jeshi la Magereza limeanzisha **Madawati ya Jinsia 153** ili kuwezesha uwepo wa fursa sawa za kijinsia na kupambana na vitendo vya ukatili katika taasisi hiyo na kuzuia ukatili kwa wafungwa wakiwemo watoto walio kwenye magereza. Pia, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imeanzisha Dawati la Jinsia kwa ajili ya kushughulikia masuala ya rushwa ya ngono. Katika kipindi cha Machi 2019 hadi Machi 2020, majalada ya kesi 31 yalipokelewa kutoka katika mikoa 15. Kati ya majalada hayo, 14 yalipelekwa mahakamani na majalada 17 yanaendelea na uchunguzi.

**Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali**

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili yachangie katika kuleta maendeleo kwa Taifa. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,403 yalisajiliwa na kupatiwa vyeti cha usajili. Usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali umeongezeka kutoka mashirika 404 mwaka 2005 na kufikia mashirika 10,446 Machi, 2020.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia sheria, taratibu, mila na desturi za nchi, Wizara imewezesha marekebisho ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na. 3/2019 pamoja na kutunga kanuni tatu zenye lengo la kuweka mazingira wezeshi ya utekelezaji wa Sheria hiyo.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika ngazi ya mikoa na Halmashauri, Wizara imewezesha uteuzi wa **Wasajili Wasaidizi (Maafisa Maendeleo ya Jamii) 211** katika ngazi ya mkoa na Halmashauri wakiwemo Wasajili Wasaidizi 26 kutoka katika mikoa na 185 kutoka katika Halmashauri.

**F. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI CHINI YA IDARA KUU YA MAENDELEO YA JAMII (FUNGU 53)**

**57** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara yangu imeendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Taasisi ya Ustawi wa Jamii. Kwa kifupi naomba nitambue yafuatayo:-

**Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru**

**58** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru imeendelea kutoa mafunzo ya maendeleo ya jamii katika ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamili. Katika mwaka 2019/20, Taasisi ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi 2,254,210,000 ambapo hadi kufikia Machi 2020, Taasisi iliweza kukusanya shilingi 1,664,186,824.37 sawa na asilimia 74 ya makadirio. Aidha, Taasisi ilidahili jumla ya wanafunzi 1,971 katika fani ya maendeleo ya jamii ikilinganishwa na wanafunzi 628 waliodahiliwa mwaka 2016/17 sawa na ongezeko la asilimia 213.85. Vilevile, mwaka 2019/20, wanafunzi 917 walihitimu katika fani na ngazi mbalimbali ikilinganishwa na wanafunzi 200 waliohitimu mwaka 2016/17.

**59** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019/20, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru imeanzisha programu ya kukuza vipaji vya wanafunzi. Taasisi imeanzisha Kituo cha Kidigitali cha Ubunifu kijulikanacho kama **Jamii Outreach Digital Innovation Centre (JODIC)** mwezi Novemba, 2019 kwa ajili ya kuatamia na kuboresha mawazo ya ubunifu ili kutatua changamoto zinazoikabili jamii. Kituo hiki kitawasaidia wanafunzi kufikiri na kuboresha mawazo yao na kuyaweka kwa vitendo. Kituo hicho kitasimamia maeneo makuu matatu ambayo ni: Ushirikishwaji Jamii; Uanagenzi; na Ubunifu wa Kidijitali.

**Taasisi ya Ustawi wa Jamii**

**60** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Ustawi wa Jamii imeendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada, Stashahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamili. Katika mwaka 2019/20, Taasisi ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi 9,270,372,000 ambapo hadi Machi 2020, Taasisi iliweza kukusanya shilingi 6,054,913,160 sawa na asilimia 65.31 ya makadirio. Aidha, Taasisi ilidahili wanafunzi 1,799 mwaka 2019/20 ikilinganishwa na wanafunzi 1,246 waliodahiliwa mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 44.38. Vilevile, katika mwaka 2018/19, jumla ya wanafunzi 1,541 walihitimu masomo katika fani na ngazi mbalimbali ikilinganishwa na wanafunzi 1,172 waliohitimu mwaka 2016/17.

**61** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha mafunzo yanayotolewa na Taasisi yanawajengea uwezo wahitimu kujiajiri au kuajirika, Taasisi imeanzisha programu ya uanagenzi (apprenticeship) inayolenga kuwajengea wanafunzi na wahitimu uzoefu katika ajira. Taasisi imeshatambua na kufanya mazungumzo na waajiri ambao watawapokea wanafunzi na wahitimu kwa kipindi cha miezi mitatu ikiwa ni sehemu yao ya kujifunza wakiwa kazini chini ya uangalizi maalum. Aidha, Taasisi ya Ustawi wa Jamii imeendelea kukuza ubunifu wa wanafunzi ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao baada ya kuhitimu mafunzo. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Taasisi imeanzisha Ukumbi wa Ubunifu (ISW Digital Innovation Hub). Lengo la ukumbi huu ni kuwapa wanafunzi nafasi ya kuibua ubunifu katika nyanja mbalimbali.

**G. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA BAJETI YA MAPATO, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2020/2021**

**IDARA KUU YA AFYA - FUNGU 52**

**62.** ***Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21 Wizara kupitia Fungu 52 (Idara Kuu ya Afya) imejiwekea vipaumbele vifuatavyo ili kuboresha huduma za afya nchini:-

i. Kuendelea kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za chanjo ili kuwakinga watoto chini ya miaka 5, akina mama wajawazito na kutoa chanjo nyinginezo za kimkakati za kukinga na kudhibiti ya magonjwa yanayozuilika kama Homa ya Ini, kichaa cha mbwa na mengineyo;
ii. Kuimarisha Huduma za Lishe na Kuboresha Usafi wa Mazingira nchini;
iii. Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa yanayoambukiza ikiwa ni pamoja na Malaria, Kifua Kikuu na UKIMWI pamoja na magonjwa yasiyoambukiza kama vile magonjwa ya moyo, kisukari na saratani;
iv. Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini;
v. Kupunguza vifo vya akina mama na watoto wachanga vinavyotokana na uzazi;
vi. Kuimarisha utoaji wa huduma za afya za kibingwa na ubingwa bobezi;
vii. Kuendelea kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma katika Hospitali ya Taifa, Maalumu, Rufaa za Kanda na Mikoa;
viii. Kuimarisha mpango wa Taifa wa utayari wa kukabiliana na magonjwa ya milipuko, ajali na majanga; na
ix. Kuimarisha mafunzo na maendeleo ya wataalam katika Sekta ya Afya.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza vipaumbele vilivyoanishwa katika mwaka 2020/21, Wizara imekadiria kutumia kiasi cha **shilingi bilioni 900**. Baadhi ya maeneo yaliyotengewa fedha kwa mwaka 2020/21 ni pamoja na: -

i. Ununuzi na usambazaji wa chanjo shilingi bilioni 51.5 zimetengwa;
ii. Kupunguza Vifo vya akina Mama vitokanavyo na Uzazi na vifo vya Watoto, jumla ya shilingi bilioni 3.5 zimetengwa kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa vituo 6 vya kukusanyia Damu Salama (Satellite Blood Banks), katika mikoa yenye uhitaji mkubwa;
iii. Ununuzi na Usambazaji wa Dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi ambapo shilingi bilioni 246 zimetengwa ambapo kati ya fedha hizo shilingi bilioni 46 ni kwa ajili ya Miradi Misonge ambayo ni UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu;
iv. Kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma katika Hospitali ya Taifa, Hospitali Maalumu, Hospitali za Rufaa za Kanda na Hospitali za Rufaa za Mikoa, shilingi bilioni 28 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa miundombinu katika Hospitali hizo;
v. Kuendelea kuimarisha huduma za kibingwa na ubingwa bobezi katika Hospitali ya Taifa, Hospitali Maalum, na Hospitali za Rufaa za Kanda ambapo, kiasi cha shilingi bilioni 12.5 kimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa tiba;
vi. Kukabiliana na magonjwa ya milipuko, ajali na majanga ambapo shilingi milioni 440 zimetengwa; na
vii. Kuboresha miundombinu ya vyuo vya afya na kugharamia mafunzo na maendeleo ya wataalam katika Sekta ya Afya, kiasi cha shilingi bilioni 19 zimetengwa kwa ajili ya kugharamia mitihani, chakula na ukarabati wa miundombinu vya Vyuo vya Afya.

**IDARA KUU YA MAENDELEO YA JAMII - FUNGU 53**

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Wizara kupitia Fungu 53 itatekeleza vipaumbele vifuatavyo ili kuboresha utoaji huduma za ustawi wa jamii na maendeleo ya jamii:-

i. Kukuza ari ya jamii kushiriki katika kujiletea maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa kutumia nguvu kazi na rasilimali zinazowazunguka;
ii. Kuwezesha Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru kuboresha utoaji wa mafunzo yanayokidhi mahitaji ya soko na kutekeleza dhana ya uanagenzi;

# HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII JINSIA WAZEE NA WATOTO

iii. Kuwezesha Vyuo vya Maendeleo ya Jamii kuboresha utoaji wa mafunzo yanayokidhi mahitaji ya soko na kutekeleza dhana ya uanagenzi;
iv. Kuwezesha Taasisi ya Ustawi wa Jamii kuboresha utoaji wa mafunzo yanayokidhi mahitaji ya soko;
v. Kupambana na kutokomeza ukatili na udhalilishaji dhidi ya wanawake, wazee na watoto ikiwa ni pamoja na kudhibiti wimbi la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani;
vi. Kuratibu na kuweka mazingira wezeshi ya kuendeleza huduma atamizi za uwezeshaji kiuchumi kwa makundi ya jamii yakiwemo wanawake na vijana;
vii. Kuhakikisha uingizwaji wa masuala ya jinsia ikiwa ni pamoja na kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi za maamuzi;
viii. Kuratibu kampeni ya kuhamasisha jamii kubadili mtazamo katika kutumia fursa mbalimbali za kiuchumi kwa kukuza ajira kwa wanawake na makundi mengine katika jamii;
ix. Kuweka na kuendeleza mifumo imara ya kijamii katika malezi, ulinzi na maendeleo ya familia na mtoto;
x. Kuimarisha uratibu na uanzishaji wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na vituo vya kijamii vya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto;
xi. Kuwezesha upatikanaji wa huduma na mahitaji ya msingi kwa makundi yenye uhitaji maalum ikiwemo wahanga wa majanga makubwa, wazee na watoto; na
xii. Kuimarisha ufuatiliaji na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili yaweze kutoa mchango chanya katika ujenzi wa Taifa.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza vipaumbele vilivyoanishwa kwa mwaka 2020/21, Wizara kupitia Fungu 53 imekadiria kutumia kiasi cha **shilingi bilioni 33** kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali ya Wizara ikiwa ni pamoja na uendeshaji wa ofisi na miradi ya maendeleo. Baadhi ya maeneo yaliyotengewa fedha kwa mwaka 2020/21 ni pamoja na:-
i. Kujenga kumbi pacha na hosteli katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru ambapo jumla ya shilingi bilioni 2.7 zimetengwa;
ii. Kuboresha utoaji wa mafunzo ya taaluma ya maendeleo ya jamii ili kukidhi mahitaji ya soko na kutekeleza dhana ya uanagenzi, kukuza ujuzi wa wahitimu na kuwajengea uwezo wa kujiajiri na kuajiriwa ambapo jumla ya shilingi bilioni 6.6 zimetengwa;
iii. Kukarabati majengo na miundombinu katika makazi ya wazee ambapo jumla ya shilingi milioni 400 zimetengwa;
iv. Kujenga Shule ya Maadilisho katika Mkoa wa Geita ambapo jumla ya shilingi milioni 200 zimetengwa;
v. Kuimarisha ujenzi wa mahabusu ya watoto katika mikoa ya Kigoma na Mtwara ambapo jumla ya shilingi milioni 700 zimetengwa;
vi. Kuwezesha Taasisi ya Ustawi wa Jamii kuboresha utoaji wa mafunzo yanayokidhi mahitaji ya soko ili kukuza ujuzi wa wahitimu kwa ajili ya kupata uwezo wa kujiajiri na kuajiriwa. Jumla ya shilingi milioni 250 zimetengwa; na
vii. Kutokomeza ukatili wa kijinsia katika jamii ambapo jumla ya shilingi milioni 827.95 zimetengwa.

## H. SHUKRANI

66. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekuwa ikipata ushirikiano mkubwa kutoka nchi rafiki, Mashirika ya Kimataifa na sekta nyingine zinazosaidia na kuchangia katika huduma za Afya, Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii.

67. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua nafasi hii ya kipekee kuzishukuru nchi za Canada (DFATD), Denmark (DANIDA), na Ireland (Irish Aid), Uswisi (SDC), Korea Kusini (KOICA) na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa yakiwemo Benki ya Dunia, UNICEF, kwa kuchangia katika Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund), ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya nchini. Aidha, napenda kuzishukuru nchi za China, Cuba, India, Italia, Japan, Marekani, Misri, Sweden, Uingereza, Ujerumani na Ufaransa na nchi nyingine ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara kwa njia mbalimbali.

68. ***Mheshimiwa Spika,*** nayashukuru pia mashirika mengine ya Kimataifa kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Wizara. Mashirika hayo ni pamoja na: Mashirika yaliyo chini ya Umoja wa Mataifa (UNAIDS, UNDP, UNFPA, UN-Women, WHO na IAEA); Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU); Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); GAVI; PEPFAR; CDC; USAID; PMI; Global Fund; Abbott Fund; DFID; EED; Elizabeth Glaser Paediatric Aids Foundation (EGPAF); GIZ; Global Fund (for HIV, TB na Malaria); Bill and Melinda Gates Foundation; Good Samaritan Foundation (GSF); HelpAge International; John Snow Incorporation (JSI); JICA; KfW; Save the Children; World Vision; Benki ya STANBIC; na Walter REED.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** niwashukuru watu binafsi, vyama vya hiari na mashirika yasiyo ya kiserikali ya ndani ya nchi kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya. Mashirika hayo ni pamoja na Benjamin William Mkapa HIV/AIDS Foundation, AGOTA, Aga Khan Foundation, APHFTA, AMREF, AGPAHI, APT, BAKWATA, CSSC, CCT, Counsenuth, ELCT, Ifakara Health Institute, Lions Club, MAT, AFRICARE, Msalaba Mwekundu, MEHATA, MEWATA, TAMWA, TAWLA, TGNP, MDH, MeLSAT, PASADA, PAT, PSI, PRINMAT, Rotary Club International, SIKIKA, Shree Hindu Mandal, TANNA, TPHA, TPRI, Tanzania Surgical Assosciation (TSA), Tanzania Diabetic Association, TANESA, THPS, TUNAJALI, Tanzania Midwife Association, TDA, TAYOA, TISS, TEC, UMATI, USADEFU, White Ribbon Alliance, LSF, Kivulini, WiLDAF, TCRF na FSDT.

70. ***Mheshimiwa Spika,*** navishukuru Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam, Muhimbili, Sokoine, Ardhi, Mzumbe, Dodoma, Chuo Kikuu Huria, Kumbukumbu ya Hurbert Kairuki, IMTU, Tumaini, St. Agustino, CUHAS, Sebastian Kolowa, St. John, Aga Khan, Morogoro Muslim, Taasisi ya Teknolojia ya Nelson Mandela, Arusha pamoja na Vyuo vyote vilivyo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya na maendeleo ya jamii. Aidha, nawashukuru wadau wengine waliotoa huduma ya elimu kwa njia za redio, televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii katika masuala ya afya na maendeleo ya jamii, hususani katika mapambano dhidi ya Corona nchini.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha utendaji wangu wa kazi nikiwa Waziri, nimepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Napenda kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile (Mb.)**, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, naomba kuwashukuru **Dkt. Zainabu Chaula** aliyekuwa Katibu Mkuu (Afya) na **Dkt John K. Jingu** Katibu Mkuu (Maendeleo ya Jamii) kwa mchango wao katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yangu. Vilevile, nawashukuru **Prof. Muhammad Bakari Kambi**, aliyekuwa Mganga Mkuu wa Serikali, Makamishna, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya Wizara. Nawashukuru pia wakurugenzi wakuu wa hospitali za Taifa na Kanda ambao ni **Prof. Lawrence M. Museru** (Hospitali ya Taifa Muhimbili), **Dr. Respicious L. Boniface** (Taasisi ya Mifupa MOI), **Prof. Mohamed Janabi** (Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete), **Dr. Julius Mwaiselage,** (Taasisi ya Saratani ya Ocean Road), **Dr. Alphonce Chandika** (Hospitali ya Benjamin Mkapa), **Dr. Riziki M. Kisonga** (Hospitali ya Kibong'oto), **Dr. Erasmus E. Mdeme** (Hospitali ya Mirembe) na Wakurugenzi wa Hospitali za Rufaa za Kanda **Dr. Godlove Mbwanji** (Hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya), **Prof. Abel Makubi** (aliyekuwa Mkurugenzi wa Hospitali ya Bugando) na **Dr. Geleard Masenga** (Hospitali ya KCMC).

72. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee naomba kuwashukuru wakurugenzi na wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ambazo ni MSD, NHIF, TMDA, NIMR, Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali, TFNC, Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru pamoja na Mabaraza ya Kitaaluma na Bodi za Usajili, Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Waganga Wafawidhi wa Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati, Wakuu wa Vyuo vya Mafunzo vilivyo chini ya Wizara na wafanyakazi wote wa Wizara na Mashirika ya Dini, Mashirika ya Kujitolea na Mashirika Binafsi. Natoa shukrani kwa sekta zote ambazo tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za afya, maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano wao. Nawaasa waendelee kuzingatia misingi ya huduma bora na kufanya kazi kwa bidii kwa manufaa ya taifa letu.

73 ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii pia kuishukuru familia yangu, kwa uvumilivu wao na pia kwa kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. Kwa wananchi wa Mkoa wa Tanga nawashukuru kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kutekeleza majukumu yangu.

## I. MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA 2020/21

**Idara Kuu ya Afya - Fungu 52**

**Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2020/21**

74 ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/21 Wizara na Taasisi zilizo chini yake imekadiria kukusanya kiasi cha **shilingi 467,799,587,522 (shilingi bilioni mia nne sitini na saba, milioni mia saba tisini na tisa, laki tano themanini na saba, mia tano ishirini na mbili).** Kati ya fedha hizo, **shilingi 155,046,746,999 (shilingi bilioni mia moja hamsini na tano, milioni arobaini na sita, laki saba na elfu arobaini na sita, mia tisa tisini na tisa)** zinatarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani (Makao Makuu ya Wizara, hospitali za rufaa za mikoa, Maalum, pamoja na mabaraza). Aidha, Mashirika yaliyo chini ya Wizara yanakadiriwa kukusanya **shilingi 312,752,840,523 (shilingi bilioni mia tatu kumi na mbili, milioni mia saba hamsini na mbili, laki nane na elfu arobaini, mia tano ishirini na tatu).** Makusanyo hayo ni sawa na ongezeko la asilimia 21 ikilinganishwa na makadirio ya mwaka 2019/20 ya **shilingi 368,536,195,026**.

**Matumizi ya Kawaida**

75 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Wizara kupitia **(Fungu 52)** imepanga kutumia kiasi cha **shilingi 900,088,240,000 (shilingi bilioni mia tisa, milioni themanini na nane, laki mbili na elfu arobaini)** ili iweze kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **shilingi 539,128,874,000 (shilingi bilioni mia tano thelathini na tisa, milioni mia moja ishirini na nane, laki nane na sabini na nne elfu)** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 58** ya bajeti ya Fungu 52, ambapo kiasi cha **shilingi 357,565,924,000 (shilingi bilioni mia tatu hamsini na saba, milioni mia tano sitini na tano, laki tisa na elfu ishirini na nne)** ni kwa ajili ya Mishahara ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake, na kiasi cha **shilingi 181,562,950,000 (shilingi bilioni mia moja themanini na moja, milioni mia tano sitini na mbili, laki tisa na elfu hamsini)** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Miradi ya Maendeleo**

76 ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa shughuli za maendeleo, Wizara (Fungu 52) inakadiria kutumia **shilingi 360,959,366,000 (shilingi bilioni mia tatu sitini, milioni mia tisa hamsini na tisa, laki tatu na elfu sitini na sita)** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na **asilimia 40** ya bajeti ya Fungu 52. Kati ya hizo, fedha za ndani ni **shilingi 280,700,000,000 (shilingi bilioni mia mbili themanini na milioni mia saba)** na fedha za nje ni **shilingi 80,259,366,000 (shilingi bilioni themanini, milioni mia mbili hamsini na tisa, laki tatu na elfu sitini na sita)**

77. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2020/21 Wizara (Idara Kuu ya Afya - Fungu 52) inaomba jumla ya **Shilingi 900,088,240,000 (shilingi bilioni mia tisa, milioni themanini na nane, laki mbili na elfu arobaini)**

**Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii - Fungu 53**

**Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2020/21**

78 ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Wizara imekadiria kukusanya **shilingi 5,347,250,000 (shilingi bilioni tano, milioni mia tatu alobaini na saba, laki mbili na elfu hamsini)** kutokana na ada na tozo mbalimbali za usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, mapato ya ada za mitihani na uuzaji wa mitaala ya Mafunzo ya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii na mapato mengine.

**Matumizi ya Kawaida**

79. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/21, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha **shilingi 26,491,375,000 (shilingi bilioni ishirini na sita, milioni mia nne tisini na moja, laki tatu na elfu sabini na tano)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **shilingi 12,842,081,000 (shilingi bilioni kumi na mbili, milioni mia nane arobaini na mbili na elfu themanini na moja)** ni Mishahara ya watumishi na **shilingi 13,649,294,000 (shilingi bilioni kumi na tatu, milioni mia sita arobaini na tisa, laki mbili na elfu tisini na nne)** ni Matumizi Mengineyo.

**Miradi ya Maendeleo**

80. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa shughuli za maendeleo, Wizara inakadiria kutumia **shilingi 6,704,364,000 (shilingi bilioni sita, milioni mia saba na nne, laki tatu na elfu sitini na nne)** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **shilingi 4,000,000,000 (shilingi bilioni nne)** ni fedha za ndani na **shilingi 2,704,364,000 (shilingi bilioni mbili, milioni mia saba na nne, laki tatu na elfu sitini na nne)** ni fedha za nje.

81 ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2020/21, Wizara (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii - Fungu 53) inaomba jumla ya **shilingi 33,195,739,000 (shilingi bilioni thelathini na tatu, milioni mia moja tisini na tano, laki saba na elfu thelathini na tisa)**

82. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya fedha zote zinazoombwa na Wizara kwa Mafungu yote (Fungu 52 na 53) ni **shilingi 933,283,979,000 (shilingi bilioni mia tisa thelathini na tatu, milioni mia mbili themanini na tatu, laki tisa na elfu sabini na tisa).**

| Na. | Fungu | Matumizi ya Kawaida | Miradi ya Maendeleo | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Fungu 52 | 539,128,874,000 | 360,959,366,000 | 900,088,240,000 |
| 2 | Fungu 53 | 26,491,375,000 | 6,704,364,000 | 33,195,739,000 |
| | **Jumla** | **565,620,249,000** | **367,663,730,000** | **933,283,979,000** |

83. ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto *www.moh.go.tz* na ***www.jamii.go.tz.***

84. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.





# Wanawake kukataa unyanyasaji watoto, watu wenye ulemavu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANAWAKE katika Halmashauri wa Wilaya ya Mbeya wameapa kusimamia na kutekeleza wajibu wao ndani ya jamii, ikiwamo kutokubaliana na vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya watoto pamoja na wenye ulemavu.

Hayo yalisema na Mwenyekiti wa Vituo vya Taarifa na Maarifa, Flora Mlowezi, alipokuwa akizungumza na Nipashe, ambapo alisema miongoni mwa masuala wanayoyafanyia kazi hivi sasa ni mapambano dhidi ya unyanyasaji kwa wenye ulemavu na watoto.

Alisema katika kukabiliana na suala hilo, wanaendelea kutoa elimu kupitia vyombo mbalimbali vya habari zikiwamo redio juu ya madhara ya vitendo hivyo na kuwasisitiza watoto na wenye ulemavu kuripoti kwenye vyombo vya sheria.

"Ni muhimu pia kujadili maendeleo na vikwazo vinarudisha nyuma jitihada zetu katika kudhibiti vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya watu wenye ulemavu," alisema na kuongeza:

"Ni wazi sasa tumeanza kuona mabadiliko katika nyanja mbalimbali za kielimu, afya, maji na kilimo, lakini bado tunaendelea na vita dhidi ya vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na wenye ulemavu."

Alisema mbali na kukabiliana na vitendo vya ukatili, pia wamebeba ajenda ya uchaguzi kupitia ilani ya wanawake ya mwaka 2019/2020 iliyozinduliwa mwaka 2019 na Mtandao wa Jinsia Tanzania TGNP, ambayo ndani yake imeeleza mikakati ya 50/50 ya mwanaume na mwanamke katika uongozi wa mwaka huu.

Alifafanua kuwa ilani hiyo imetoa dira kwa wanawake kugombea nafasi mbalimbali za uongozi wakiwa wanabeba ajenda za maendeleo zenye kukubalika.

Diwani wa Kata ya Mshewe, Esther Mbega, alisema yeye ni miongoni mwa wanawake walioipigwa vita wakati anagombea nafasi ya udiwani mwaka 2015.

Alisema licha ya vitisho na kejeli, alisimamia ajenda za maendeleo na hatimaye akamshinda mshindani wake, ambaye alikuwa ni mwanaume.

# Watendaji kata, vijiji Mbarali waelekezwa elimu ya corona

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MKUU wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Reuben Mfune, ametoa maelekezo kwa watendaji wote wa kata na vijiji kuhakikisha wanafikisha elimu ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa Covid-19 kwa kila mwananchi.

Mfune alisema haridhishwi na kasi ya utoaji elimu kutoka kwa watendaji hao na kwamba wajipange upya sasa kuhakikisha wanawafikia wananchi wa kila eneo wilayani humo.

Aliyasema hayo juzi wakati wa kikao maalum cha kamati ya mapambano ya virusi vya corona ambayo inaundwa na baadhi ya viongozi.

Aidha, aliagiza gesti bubu zote zifungwe sambamba na kuzuia michezo ya drafti, bao pamoja na michezo mingine inayokusanya watu ili kuzuia maambukizi.

"Baadhi ya watendaji wa serikali wakiwamo watendaji wa kata, vijiji, hawawajibiki ipasavyo katika kutoa maelekezo yanayotolewa na serikali dhidi ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona, hali inayozua taharuki kwa wananchi kwa sababu wanapata taarifa ambazo sio za kweli," alisema Mfune.

Mfune aliongeza kuwa kamati iliyoundwa kwa ajili ya kufuatilia maelekezo yanayotolewa na viongozi wa nchi, imefanya ufuatiliaji kwenye kata saba na kubaini kuwa baadhi ya watendaji hawatekelezi vizuri majukumu yao dhidi ya janga la corona.

Aliwaagiza madereva wa vyombo vya moto pamoja na wananchi wote wilayani humo kuvaa barakoa wanapokuwa kwenye mikusanyiko au misongamano.

Kadhalika, aliwaomba mafundi vyerehani wanaoshona barakoa kutumia vitambaa vilivyoelekezwa na wataalamu wa afya ambavyo vitasaidia kupunguza kasi ya maambukizi, lakini wauze kwa bei nafuu.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Tulia Trust, Jacqueline Boaz (kulia), akimkabidhi ndoo 100 za maji Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Gregory Emmauel, kwa ajili ya kunawia mikono kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona. Ndoo hizo zitasambazwa maeneo mbalimbali, ikiwamo sokoni na stendi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# NEC kuchukua hadhari ya corona uboreshaji daftari

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imesema kuwa imechukua tahadhari zote muhimu katika kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa hatari wa Covid-19, wakati wa mchakato wa uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura kwa awamu ya pili katika mikoa ya Mbeya na Songwe.

Akizungumza na Nipashe jana jijini Mbeya, Ofisa Habari Mwandamizi wa NEC, Abdulwakili Saiboko, alisema mchakato wa uboreshaji wa daftari la kudumu kwa wapigakura kwa awamu ya pili katika mikoa ya Mbeya na Songwe utafanyika kuanzia kesho hadi Mei 5, mwaka huu.

Saiboko alisema katika vituo vyote ambavyo zoezi litafanyika, Tume itahakikisha kunakuwa na maji tiririka ya kunawa, vitakasa mikono pamoja watumishi watakaokuwa wanatoa huduma kuvaa barakoa.

Alisema mashine ambazo zimeletwa kutoka jijini Dar es Salaam kwa ajili ya mchakato huo zitapuliziwa dawa ya kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona, akisema lengo ni kuhakikisha hakuna maambukizi yatakayoathiri kazi hiyo.

"Kwa sababu watu watakuwa wanaweka vidole kwenye mashine kwa ajili ya kuhakikiwa, pembeni tutakuwa na dawa ya kusafisha mashine ili kuua vijidudu ikiwamo virusi... kila mtu mmoja akiweka kidole tutakuwa tukisafisha, na kila kituo kitakuwa na maji tiririka pamoja na sabuni," alisema Saiboko.

Aliongeza kuwa ili kupunguza misongamano, mwananchi anaweza kuhakiki taarifa zake kupitia simu yake ya kiganjani ambapo anaweza kuandika *152*00# na kupata menyu kuu ambayo itamuongoza kwenye mtiririko wa kupata taarifa zake.

Alisema kwa sasa idadi kubwa ya vijana wanatumia mitandao ya kijamii, hivyo wameandaa utaratibu wa kuhakikisha wanahakiki taarifa zao kupitia tovuti ya NEC.

Ofisa Utumishi Mwandamizi wa NEC, Hidaya Gwando, aliwashauri wananchi kutumia njia ya mtandao kuhakiki taarifa zao ili kuepusha misongamano, huku akiwataka kutumia muda huo uliowekwa ili wapate haki yao ya kikatiba ya kushiriki kwenye uchaguzi mkuu ujao, ambao unatarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwaka huu.



# Zanzibar yamlilia Jaji Ramadhani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

UONGOZI wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Zanzibar, umesema umepokea taarifa za kifo cha mmoja wa kiongozi wake, Mchungaji Jaji Mkuu mstaafu, Augostino Ramadhan, kwa masikitiko makubwa na majonzi.

Askofu wa kanisa hilo Zanzibar, Dk. Michael Hafidh, alisema mchango wa Jaji Mkuu mstaafu Ramadhan katika kanisa hilo ni mkubwa ikiwamo katika kujenga waumini vijana uadilifu, kupenda kanisa na kumcha Mungu katika kipindi chote.

Alisema uadilifu wake na kupenda kanisa ulimfanya kupanda ngazi hatua kwa hatua katika kanisa hilo hadi kufikia cheo cha mchungaji.

"Uongozi wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Zanzibar umesikitishwa na kifo cha aliyekuwa kiongozi muadilifu wa kanisa hilo na muumini wake hayati Augostino Ramadhani...kanisa litaendelea kumkumbuka kutokana na mchango wake mkubwa katika kulifanya kuwa taasisi imara muda wote na kuheshimika mbele ya wafuasi wake ndani na nje ya nchi," alisema.

Monica Mossi Kassim, mkufunzi wa kwaya kanisani hapo, alimtaja marehemu kuwa ni miongoni mwa walimu wa kwaya kanisani ambaye alichukua nafasi hiyo kutoka kwa walimu waliobobea akiwamo marehemu Ernest Wakati.

Aidha, alisema marehemu alikuwa mtaalamu aliyebobea katika kupiga kinanda katika kanisa kipindi chote alipokuwapo Zanzibar.

Jaji Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu, alimtaja Jaji Ramadhani atakumbukwa kutokana na mchango wake mkubwa wa kuleta mageuzi katika Mahakama pamoja na mabadiliko ya watumishi na usikilizaji wa kesi.

Alisema baada ya kuteuliwa kuwa jaji mkuu katika mwaka 1982 na aliyekuwa Rais wa awamu ya pili, Hayati Aboud Jumbe, aliweka utaratibu mzuri wa vyeo kwa majaji pamoja na mahakimu na kuja na mfumo wa utumishi unaofahamika kwa wakati ule.

Alisema aliifanya mahakama hiyo kufanya kazi zake kutoka katika mazoea na kufuata misingi ya sheria na taaluma zaidi, mabadiliko ambayo yaliijengea hadhi taasisi hiyo ambayo ni sehemu ya muhimili wa dola.

"Tumeondokewa na aliyekuwa Jaji Mkuu wa kwanza mzalendo Ali Haji Pandu ambaye alijenga misingi ya taasisi hiyo pamoja na uendeshaji wake, lakini tumeondokewa na marehemu Augostino Ramadhani aliyefanya kazi kubwa kujenga taasisi hiyo katika kipindi cha mabadiliko," alisema.

Ramadhani alizaliwa Zanzibar Desemba 28 mwaka 1945 huko Kisimamajongoo na kupata elimu yake ya msingi na sekondari katika shule mbalimbali zilizopo Tanzania Bara hadi ilipofika mwaka 1966 alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam kusomea fani ya sheria na kuhitimu mwaka 1970.

Mwaka 1970 alijiunga katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) akiwa raia na baadaye kupata mafunzo mbalimbali ya kijeshi na kumfanya miongoni mwa askari walioshiriki katika vita vya kumng'oa nduli Iddi Amin aliyeivamia ardhi ya Tanzania katika mwaka 1979.

Alipokuwa nchini Uganda alikuwa akiendesha kesi za Mahakama ya kijeshi zinazowahusu wapiganaji.


Mapema katika mwaka 1978, Jumbe alimteua Ramadhani kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Zanzibar, huku akifanya kazi na Jaji mstaafu Damian Lubuva ambaye kwa wakati huo alikuwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar.

Katika mwaka 1982 aliteuliwa kushika wadhifa wa jaji mkuu wa Zanzibar, huku akiwa na cheo cha Luteni Kanali katika JWTZ.

Juni 23, 1989 aliyekuwa Rais wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, alimteua kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani Tanzania, hivyo nafasi ya Jaji Mkuu wa Zanzibar kuchukuliwa na Jaji Hamid Mahmoud.

Aidha, Ramadhan aliteuliwa kuwa Kamishna wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) katika mwaka 2002 na Rais Amani Abeid Karume akiwa Makamu Mwenyekiti.

"Kupiga kinanda ni sehemu ya ibada...napenda kupiga kinanda na uteuzi wa Jaji Mkuu wa Serikali ya Muungano kamwe haukusitisha kufanya kazi yangu ninayoipenda ya kupiga kinanda...hata nilipoteuliwa kuwa Jaji Mkuu wa Zanzibar nilikuwa nikipiga kinanda kama kawaida wakati nikipata nafasi kwenda kanisani," aliwahi kusema wakati wa uhai wake.




Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Balozi Seif Ali Idd, akipokea mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 30 kutoka kwa Ofisa Mkuu wa Biashara wa Benki ya CRDB, Dk. Joseph Witts, ikiwa ni mchango wa benki hiyo kusaidia jitihada za serikali katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtalii afa kwa kugonga boti

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIA wa Canada, Kevin Nilas (34), amefariki dunia baada ya kugonga boti ya wavuvi wakati akicheza mchezo wa kujirusha baharini huko Paje Wilaya ya Kusini Unguja.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Unguja, Ramadhan Khamis Salmin, alithibitisha kutokea kwa kifo hicho, na kuwa Kevin ni mtalii aliyekuwa akicheza mchezo wa kujirusha baharini kwa kusaidiwa na mawimbi ya bahari.

Alisema mtalii huyo wakati akicheza mchezo huo aligongana na boti ya wavuvi waliokuwa wakifanya shughuli za uvuvi na kujeruhiwa sehemu mbalimbali za mwili na kusababishia kifo chake.

"Tulipokea taarifa ya ajali ya mtalii Kevin mchana baada ya kugongwa na boti ya wavuvi waliokuwa wakirudi katika shughuli zao za uvuvi...alipata majereha makubwa sehemu ya kichwa na kusababisha kifo chake," alisema.

Kamanda Salmin alisema juhudi za kuwasiliana na jamaa zake ukiwamo ubalozi wa Canada nchini kwa ajili ya kusafirishwa maiti hiyo zinafanywa.

## SMZ yapewa mil. 30/- za corona

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BENKI ya NMB imetoa msaada wa Sh. milioni 30 kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) katika kuunga mkono jitihada za serikali katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa (Covid-19).

Akikabidhi msaada huo Meneja wa NMB Zanzibar, Abdala Duchi, alisema benki hiyo imekuwa ikisaidia jamii na serikali kila inapotokea haja ya kufanya hivyo, ikiwa ni uungaji mkono juhudi za serikali katika kuwapatia maendeleo wananchi wake sambamba na kuwasaidia pale yanapotokea majanga mbalimbali.

Duchi alisema NMB imekuwa mstari wa mbele kutoa msaada kila inapotokea haja ya kufanya hivyo, kwa kuamini kuwa afya njema ni jambo la kwanza katika maisha ya kila siku.

"Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Idd, leo tupo hapa kukabidhi hundi ya mfano ya Sh. milioni 30, ikiwa tayari fedha tushaziingiza kwenye akaunti husika kama maelezo ya serikali yalivyotolewa" alisema Duchi.

Alimhakikishia Balozi Idd kuwa benki hiyo ipo tayari wakati wowote kutoa msaada pale kutakapokuwa na haja ya kufanya hivyo ikiwa ni utaratibu wake, Balozi Idd alisema NMB ni miongoni mwa benki bora na yenye kujali jamii kwa kutoa misaada mbalimbali.

Balozi Iddi alisema NMB imekuwa ikitumia faida yake vizuri pale inaposaidia jamii katika masuala mbalimbali kwa lengo la kuiletea maendeleo jamii husika.

Aidha, aliipongeza benki hiyo kwa msaada wake iliyoutoa wa Sh. milioni 30 ikiwa ni katika kupambana na ugonjwa wa COVID 19.

"Niwapongeze viongozi wote wa benki hii kwa kujali na kutoa uamuzi wa kutoa msaada huu wa shilingi milioni thelathini, ni uamuzi mzuri ambao utaweza kuisaidia serikali katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Covid 19, tunaomba mwendelee kutusaidia kila inapotokea nafasi ya kufanya hivyo," alisema Balozi Iddi.

Alisema ni vyema wananchi wakafuata maelekezo ya wataalamu wa afya katika kujikinga na maradhi hayo ya corona ambayo yameikumba dunia nzima.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**WANAHITAJIKA WAFANYAKAZI**
Wanahitajika wasichana wa kuuza Duka na wa kazi za ndani , Wanahitajika haraka sana. Piga Simu namba : **0715 431528 au 0784 431528**


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA VYETI



**ELIZABETH YUDA URIA** anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0205-0045 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la taifa mwaka 2014 katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Kibosho na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S4692-0678 kilichotolewa na Baraza la mithihani la taifa mwaka 2017 katika Shule ya Sekondari St. Joseph..Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa Ya Polisi:
**DAR/MAG/RB/209161/2020**

157215

## KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI

Hati nambari: **15059 LR MWANZA.**
Mmiliki aliyeandikishwa: Cornelis Hendrik Van Vianen msimamizi wa Mirathi ya Jane Gervas Kamkala wa S.L.P 3164, Mwanza.

Muombaji:Cornelis Hendrik Van Vianen msimamizi wa mirathi ya Jane Gervas Kamkala wa S.L.P 3164, Mwanza.
Ardhi: L.O.Na. 222609 Kiwanja Na 188 &189 kitalu X Capri – point Mwanza City.

Eneo: 2,829 mita za mraba
TAARIFA IMETOLEWA: Kwamba hati ya kumiliki Ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi chochote kwa muda wa mwezi mmoja tokea tarehe ya taarifa hii.

HATI ya Asili ikionekana irudishwe
Ofisi ya Msajili wa Hati, S.L.P 1101, Mwanza.

Pia taarifa imetolewa
Polisi kwa Kumb:
**MWA/KIR/RB/335793/2020.**

157264

IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
IN THE DISTRICT REGISTRY
AT MUSOMA
MISC. LAND APPEAL NO 6 OF 2020

(Original land application no 14 of 2019 of Tarime District land and Housing Tribunal)

MASOBHU SAMWELI………………APPELLANT
VERSEUS
THEREZA MARWA NTOLA…………RESPONDENT

TO: THEREZA MARWA NTOLA

**NOTICE OF DATE OF HEARING**

TAKE NOTICE: that the above case has been fixed for hearing on 5th May, 2020 at 9:00 am before Hon. E.S. Kisanya Judge.

You are required to appear in this court on the fixed date without fail.

Given under my hand and seal of the court this 8th day of April 2020

DEPUTY REGISTRAR
MUSOMA

157262

## KUPOTEA KWA KADI YA TRACTOR

**MARTIN ZAKARIA KIBAJA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Tractor yenye namba za usajili T 136 AY aina ya SONALIKA TRACTOR.
Engine: 4100PL72E119732.
Chassis: 122BDY119197/3.
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**MUH/RB/4146/2019.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA KANDA YA SHINYANGA**

**MAOMBI YA ARDHI NAMBA 40 YA 2018**

**SHAURI ASILIA LA ARDHI NAMBA 20 YA 2016 KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MASWA.**

**BUCHAMBI MSOBI………………………………………MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**JILALA MAGASHI AMBAYE NI MSIMAMIZI WA MIRATHI YA SHABAN NYANDA……………….. …..MJIBU MAOMBI**

**KWA; JILALA MAGASHI**

**TAARIFA YA KUITWA SHAURINI**

UNAJULISHWA KWAMBA MNAMO TAREHE 16/06/2020 SAA 3;00 ASUBUHI SHAURI TAJWA HAPO JUU LIMEPANGWA KUSIKILIZWA MBELE YA MHE JAJI E.Y. MKWIZU.
HIVYO UNA AMRIWA KUHUDHULIA SIKU HIYO KATIKA MAHAKAMA KUU YA SHINYANGA BILA KUKOSA, ENDAPO HUTAHUDHULIA MAOMBI HAYO YATASIKILIZWA NA KUTOLEWA UAMUZI BILA WEWE KUWEPO.
HATI HII IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA KUPIGWA CHAPA YA MAHAKAMA LEO TAREHE 28/04/ 2020.
E.G RUJWAHUKA
NAIBU MSAJILI MAHAKAMA KUU YA TANZANIA KANDA YA SHINYANGA

NB;HII NI SEHEMU YA KUWEKA MHURI WA MAHAKAMA NA JILA LA NAIBU MSAJILI NA SAHIHI YAKE

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA YA SHINYANGA

215726302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**KANDA YA MWANZA**

**SHAURI LA ARDHI RUFAA NAMBA 73 OF 2019**

**SIMEO BUNALI……………………………MLETA RUFAA**

**DHIDI YA**

**JOSEPH MALYENGETE& 3 OTHERS…………………………………..WAJIBU RAFAA**

KWA:
1. **JOSEPH MALYENGETE**
2. **MASEBU NKONDO**
3. **KADILANHA MANYANDODI**
4. **MASHAKA FULANO**

**KUITWA SHAURINI**

Mnaarifiwa kuhudhuria hapa mahakamani tarehe 21/05/2020, kuja kusikiliza shauri la ardhi rufaa iliyofunguliwa na mwomba rufaa dhidi yenu.
Mnatahadharishwa kuwa endapo hamtafika siku hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja dhidi yenu na kutolewa maamuzi.
Hati hii imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya mahakama leo hii tarehe 27/03/2020.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MWANZA

115726102


***Kwa Habari Motomoto***

***usikose Gazeti lako la Nipashe***

***kila siku Tupigie 0782253676***



**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Watu 29 wafariki kwa mafuriko

**NAIROBI,** Kenya

WATU 800,000 hawana sehemu ya kuishi, huku 29 wakifariki kufuatia mvua kubwa kunyesha na kusababisha mafuriko na maporomoko ya ardhi.

Baadhi ya maziwa na mito pia imefurika na kuzua hofu ya mlipuko wa magonjwa.

Ziwa Nakuru na Ziwa Naivasha yameongezeka kina kulikosababishwa na mvua hizo.

Ziwa Victoria na mito Tana na Nzoia ni miongoni mwa maeneo yaliyofurika na kusababisha uharibifu wa makazi, miundombinu na mashamba katika maeneo tofauti nchini Kenya yakiwamo Kisumu, Busia, Bomet, Kericho, Narok, Naivasha na Garissa.

Mafuriko hayo pia yamesababisha maelfu ya watu kuyahama makazi yao.

Shirika la msalaba mwekundu nchini Kenya limeeleza kuwa watu 29 wamefariki kufuatia maporomoko ya ardhi.

Mtaalamu wa masuala ya mazingira, Jackson Rain, alisema uharibifu wa misitu unachangia pakubwa maziwa kujaa maji.

"Maziwa haya yako kwenye sehemu ya chini zaidi ya vyanzo vya maji na ukumbuke kwamba vyanzo hivi vimeharibiwa sana," alisema Rain na kuongeza:

"Kati ya asilimia 50 ya misitu tuliyokuwa nayo mwaka 2,000, sasa tuna asilimia saba ya misitu, kwa sababu ya watu kupewa makazi katika maeneo hayo. Zamani misitu hii ingeyakusanya maji wakati wa mvua nyingi na kuyaachilia pole pole, lakini sasa mvua inaponyesha maji hayo yanashuka kwa haraka mitoni hadi kwenye maziwa," alisema Rain.

Alisema wanawake, watoto, wazee na wagonjwa ndiyo walio hatarini zaidi, waathirika hawa sasa wakiwa wamechukua hifadhi katika shule mbalimbali.

Alisema hali hiyo inazua hofu ya mlipuko wa magonjwa kama vile kipindupindu.

Gavana wa Busia, Sospeter Ojamong, alisema serikali imeanza kutoa msaada wa dawa za kuwakinga na magonjwa hayo ikiwa ni pamoja na kuwapa msaada wa vyakula, blanketi na mahitaji mengine muhimu.

Eric Ogada, mkazi wa Nakuru anaikosoa serikali kwa kutoshughulikia janga hilo kwa wakati mwafaka akisema suluhu la kudumu inahitajika kuyanusuru maisha ya Wakenya wengi.

Tahadhari ya Idara ya Utabiri wa Hali ya Hewa nchini Kenya ilieleza kuwa baadhi ya mito ingevunja kingo zake, iliwafanya baadhi ya watu kuyahama makazi yao ambao bado wanasubiri msaada wa serikali. DW

# Mama awapikia mawe watoto akikosa chakula

**NAIROBI,** Kenya

MJANE mmoja nchini Kenya amewapikia watoto wake mawe, akiwadanganya kuwa ni chakula.

Mwanamke huyo aitwaye, Penina Bahati, mama wa watoto wanane anasema amelazimika kufikia hatua hiyo baada ya kutofanikiwa kupata kazi.

Alisema tangu ugonjwa wa corona ulipoingia, ameshindwa kupata kazi ambayo ingeweza kumuingizia kipato na kununua chakula kwa ajili ya watoto wake.

Mjane huyo anayeishi maeneo ya pwani ya mji wa Mombasa, anasema anaweka mawe na maji kwenye sufuria na kuyaweka motoni hadi watoto wake watakapo lala.

Kituo cha Runinga cha NTV kiliweka video kwenye mtandao ikimwonyesha mama huyo akipika mawe kwa muda mrefu hadi pale watoto wake walipopitiwa na usingizi.

"Ninafanya hivi kwa kuwadanganya, ninawaambia nawapikia chakula, lakini ukweli hakuna chakula, ninawadanganya hadi wanapopitiwa na usingizi," alisema Bahati.

Jirani na mama huyo (jina limehifadhiwa) akizungumza na BBC alisema amekuwa akimuona mama huyo akipika mawe pindi alipokwenda kumtembelea.

Alisema anawaomba wasamalia wajitokeze na kumpatia chakula mama huyo.

Hadi kufikia jana, mama huyo alikuwa akipokea pesa kupitia simu ya mkononi pamoja na kufunguliwa akaunti na jirani yake ili aweze kupata usaidizi.

**BBC**



Wabunge wa Uganda wakiwa bungeni, Rais Museveni amewaagiza wabunge hao, kuzirejesha pesa za ugonjwa wa corona walizogawana na kwamba ambaye hatarudisha atakatwa mshahara. PICHA: REUTER **PICHA: DW**

# Yoweri Museveni awatuhumu wabunge kula fedha za corona

**KAMPALA,** Uganda

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, amewashutumu vikali wabunge wa nchi hiyo kuamua kujipatia pesa zilizokusudiwa kusaidia katika kupambana dhidi ya ugonjwa wa corona.

Spika wa Bunge la Uganda, Rebecca Kadaga, aliagiza kila mbunge apokee kiasi cha dola elfu tano kutokana na mgao wa kiasi cha dola milioni tatu.

Sakata la wabunge kujipatia kiasi cha dola milioni tatu limekuwa gumzo mitandaoni tangu ilipofichuka kwamba walikuwa wanapanga kupewa pesa hizo kinyume na hali ilivyo kwa sasa.

Fedha hizo zilichangiwa na sekta binafsi ambazo zilikuwa mahususi kwa ajili ya kununua chakula kwa wakazi waliopo karantini.

Jambo la kushangaza, ni kwamba hata baada ya wabunge wawili kuwasilisha shauri mahakamani kupinga kutolewa kwa pesa hizo, Spika wa bunge alisema kuwa tayari zilikuwa kwenye akaunti zao.

Rais Museveni alitaja kitendo hicho kuwa cha aibu akiwataka wabunge waliozitumia pesa hizo kwa maslahi yao wazirudishe.

Wananchi wamewashtumu pia wabunge kwa kile walichokielezea kuwa tamaa badala ya kutoa sehemu ya mishahara yao minono kuchangia katika kukabiliana na janga la corona kama walivyofanya wanasiasa katika mataifa mengine.

Baadhi ya wabunge waliopinga hatua hiyo wakiwamo Muwanga Kivumbi na mbunge msanii Bobi Wine walielezea kuwa walisisitiza kuwa hawakufahamishwa vyema kuhusu vyanzo na matumizi ya pesa hizo.

Rais Museveni ameagiza pesa hizo zirudishwe mara moja na ambaye hatarudisha atakatwa mshahara.

Wakati huo huo, Rais Museveni alishutumu vitendo vya vyombo vya usalama kuwanyanyasa na kuwatesa wanasiasa wa upinzani kwa kutoa misaada ya chakula.

Rais Museveni alishangaa kwa nini wale wa chama tawala hawakuchukuliwa hatua sawa na hiyo. **DW**

# Apatikana baada ya kutangazwa kufa kwa corona

**QUITO,** Ecuador

MWANAMKE mmoja, Alba Maruri (74) ambaye alitangazwa amekufa kwa ugonjwa wa corona, amepatikana akiwa hai.

Familia ya Maruri, ilifahamishwa mwezi uliopita kwamba ndugu yao amefariki na kutumiwa majivu ya mpendwa wao baada ya mwili wake kuchomwa.

Lakini Maruri alipata fahamu baada ya kuwa katika hali ya kutojitambua kabisa kwa muda wa wiki tatu hospitali na kumuomba daktari ampigie simu dada yake.

Maruri alilazwa hospitalini katika mji wa Guayaquil, ambao ni mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Nchi hiyo yenye idadi ya watu milioni 17 imeathirika vibaya na ugonjwa huo ikiweka rekodi ya watu zaidi ya 22,000 waliopata maambukizi huku wengine takribani 600 wakifariki.

Familia hiyo ilizungumza na BBC na kusema walilazimika kusubiri kwa siku nne kabla ya mamlaka kuwasili nyumbani kwao na kuchukua miili hiyo.

Walisema walikuwa wamefunga miili hiyo kwa karatasi ya plastiki wakati wanasubiri, anasema Bertha, dada yake Inés'. Lakini sasa anataka kujua nini kilichotokea baada ya miili hiyo kuchukuliwa kutoka nyumbani.

"Tuliambiwa kwamba tusubiri na kuwa watazikwa muda wowote ule na mamlaka," alisema Inés'.

Alisema tangu wakati huo mamlaka haijawahi kuwasiliana nao.

Idadi kubwa ya vifo katika mji wa Guayaquil imesababisha kuporomoka kwa mfumo wa afya tangu Machi, mwaka huu.

**BBC**



# Pochettino: Kabla sijafa nataka kuinoa tena Spurs

**LONDON,** England

MAURICIO Pochettino amebainisha ana matumaini ya kupata nafasi ya siku moja kurudi Tottenham na kumalizia kazi aliyoianza.

Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Argentina alikuwa Kocha wa Spurs kwa miaka mitano, akiiongoza kumaliza kwenye nne bora kwa kipindi cha miaka minne, na msimu uliopita kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hata hivyo, hakuweza kutwaa taji lolote wakati alipokuwa pale, na klabu ilikuwa ikipambana katikati ya msimamo, na akafukuzwa Novemba mwaka jana.

Jose Mourinho kwa sasa ndiye mrithi wake, lakini Pochettino bado ana imani kwamba atarudi kuungana na Spurs siku moja, akikubali klabu hiyo "ipo ndani ya sakafu ya moyo wake".

"Ilikuwa safari ya kufurahisha ambayo ilimalizika kwa namna ambayo hakuna yeyote angependa imalizike vile," alisema Pochettino wakati akizungumza na BT Sport.

"Lakini ndani ya sakafu ya kifua changu, rohoni mwangu, moyoni mwangu, nina uhakika nitapita pale tena. Kwa uhakika kabisa, kutoka sasa tangu siku nilipoondoka klabuni pale, ndoto yangu ni siku moja kurudi pale na kumalizia kazi ambayo hatukuimaliza.

"Tulikaribia kushinda mataji. Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Ulaya, tulikaribia sana. Tukasimamishwa kwa namna ilivyotokea."

***



# Arthur hataki kuondoka Barca

**BARCELONA,** Hispania

KIUNGO wa Barcelona, Arthur hana pango wa kwenda Juventus na anataka kubakia pale Camp Nou "kwa miaka mingi."

Ripoti kutoka nchini Hispania zimebainisha kwamba, Juve wapo tayari kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil kutua pale Turin, ili ikiwezekana kuziba pengo la Miralem Pjanic, ambaye majaliwa yake klabuni hapo hayajulikani.

Gazeti la Mundo Deportivo lilidai Jumatatu kwamba, Barca imewapa ruhusa Juve kuzungumza na Arthur na vinara hao wa Serie A wanaweza kutoa ofa ya kumsajili.

Hata hivyo, Arthur, ambaye alijiunga na mabingwa hao wa LaLiga akitokea klabu ya Gremio ya nyumbani kwao mwaka 2018 kwa ada iliyoripotiwa kuwa euro milioni 39, anaona majaliwa yake bado yapo pale Katalunya.

Katika taarifa yake aliyoituma kwenye gazeti la Mundo Deportivo, alisema: "Mara zote kunakuwa na uvumi, lakini kiukweli kabisa malengo yangu yapo wazi kabisa. Kitu pekee kilichopo kwenye akili yangu ni kuendelea kubakia hapa Barcelona.

"Nina uhakika na nimeridhika. Najisikia vizuri sana hapa, nina imani kubwa na klabu na najivunia benchi lake la ufundi. Na malengo yangu ni kuendelea kucheza hapa kwa muda mrefu zaidi.

"Suala la kutakiwa na klabu nyingine ni la kawaida sana, lakini mimi akili yangu ni kucheza hapa kwa miaka mingi sana."

Arthur mwenye umri wa miaka 23, amecheza mechi 23 kwenye mashindano yote kwa Barca msimu huu licha ya kusumbuliwa na majeruhi ya mara kwa mara.



# Fabregas atoa mshahara wa miezi minne

**MONACO,** Ufaransa

NYOTA wa zamani wa Arsenal, Francesc Fàbregas anayecheza pale AS Monaco amekubali kusamehe mshahara wake wa miezi minne kwa ajili ya kuwasaidia wafanyakazi wengine wakati huu wa mlipuko wa virusi vya corona.

Kiungo huyo amechukua uamuzi huo baada ya uongozi wa klabu hiyo kutangaza kuwakata asilimia 30 ya mshahara wachezaji wake, katika kipindi hiki.

Asimilia 30 ya wachezaji wengine wa Monaco na mshahara wa miezi minne wa Fabregas, itatumika kwenye vita ya maambukizi ya virusi vya corona nchini Ufaransa, pamoja na kulipa mishahara ya wafanyakazi wengine wa klabu hiyo.

Fabregas anapokea mshahara wa pauni 130,000 kwa wiki, hivyo kwa hesabu ya mshahara wake wa miezi minne utakaopelekwa kwenye vita dhidi ya maambukizi ya virusi vya corona. Kama itakumbukwa Fabregas wakati anaondoka Arsenal kwenda Barcelona kwa dau la euro milioni 39, alikubali kulipa euro milioni 5 ili kukamilisha ada yake ambayo haikutimia kutokana na mabingwa hao wa Hispania kulipa euro milioni 34.

Fabregas alilipa kiasi hicho kutoka kwenye makato ya mshahara wake, ili akacheza pale Barcelona ambako ndiko alikolelewa katika akademi ya kukuza vipaji ya La Masia.

HABARI MICHEZO

# Messi hana shida kusaini mkataba mpya - Laporta




**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi "hatakuwa na shida" kusaini mkataba mpya pale Barcelona, kwa mujibu wa rais wa zamani wa klabu hiyo, Joan Laporta.

Majaliwa ya Messi hapo Camp Nou yamekuwa shakani kwa siku za hivi karibuni na hakuna uhakika kama ataendelea kukipiga hapo Barcelona, ambapo mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2021.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina anaweza kuondoka kwa miamba hao wa LaLiga kama mchezaji huru mwishoni mwa msimu wowote, na hivyo kuleta hofu juu ya majaliwa yake.

Lakini Laporta, ambaye anatarajiwa kugombea tena kwenye uchaguzi wa mwakani, amesema itakuwa rahisi kwa Messi kusaini mkataba mpya.

"(Messi) hatakuwa na shida kusaini mkataba mpya," amesema akiliambia gazeti la Deportes Cuatro Jumatano.

Mchezaji ambaye anahusishwa kwenda kuungana na Messi pale Barcelona ni Neymar, ambaye aliondoka klabuni hapo kwenda Paris Saint-Germain mwaka 2017.

Laporta amesema anaweza kumleta nyota huyo wa kimataifa wa Brazil hapo Camp Nou, ambako alitamba kwa misimu minne kabla ya kuondoka.

"Hawakuwa na uhakika na yeye," alisema. "Nitamrudisha kwa uhakika kabisa."

## Mbappe: Hakuna anayejua ninapokwenda

**PARIS,** Ufaransa

NYOTA wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe amesema "kila mtu anazungumza lakini hakuna anayejua" wakati uvumi wa kuhusishwa kwake kwenda Real Madrid ukizidi kukua.

Msimu wa Ligi Kuu Ufaransa wa 2019-20 umefutwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, lakini majaliwa ya Mbappe bado yametawala vichwa vya habari.

Kocha wa Madrid, Zinedine Zidane hajaficha hisia zake kwa kuvutiwa na Mbappe, ambaye anapewa nafasi kubwa mno ya kutua pale Santiago Bernabeu.

Mbappe ambaye mkataba wake na PSG unamalizika mwaka 2022 bado hajasaini mkataba mpya na alituma ujumbe kwenye ukurasa wake wa Twitter kuonyesha mahaba yake kwa mabingwa hao wa Ufaransa.

"Kila mtu anazungumza, lakini hakuna anayejua ... Nimeikumbuka timu yangu... @PSG_Inside," Mbappe aliandika kwenye Twitter.

Kabla ya mlipuko wa virusi vya corona kusimamisha Ligue 1 na michezo yote duniani, Mbappe alikuwa amefunga mabao 18 kwenye ligi hiyo na magoli 30 katika mashindano yote aliyoichezea PSG msimu wa 2019-20.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 amekuwa na heshima kubwa tangu alipotua PSG akitokea Monaco mwaka 2017, awali akitua kwa mkopo na ameshinda mataji mawili ya Ligue 1 na Kombe la Ufaransa.



# Woodward asema United itatikisa katika usajili



**MANCHESTER,** England

ED Woodward amesisitiza Manchester United itakuwa na "ushindani mkubwa" kwenye soko la usajili licha ya mlipuko wa virusi vya corona.

Makamu Mwenyekiti Mtendaji Mkuu huyo wa United amesema kwamba hivi karibuni uvumi ulibainisha kwamba klabu hazitafanya usajili wa fedha nyingi kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19.

Miamba hao wa Ligi Kuu England wamekuwa wakihusishwa na usajili wa nyota wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho na mshambuliaji wa Tottenham, Harry Kane miongoni mwa wachezaji.

Lakini Woodward amesema United wanataka kumuunga mkono kocha wao, Ole Gunnar Solskjaer kwenye soko la usajili.

"Mara zote ni kipaumbele chetu kuimarisha timu na kujenga kupitia kile Ole anachotaka hasa suala la kuleta wachezaji wakubwa," alisema akiuambia mtandao wa mashabiki wa klabu hiyo.

"Kwa uhakika kabisa, ni kweli tuna bahati ya kuwa na nguvu ya kifedha ikilinganishwa na klabu nyingi, lakini hatuwezi kusita kusema kwamba kuna athari kutokana na mlipuko wa virusi.

"Ningependa kusema kwamba, pamoja na janga hili, lakini tutaleta ushindani mkubwa kwenye soko la usajili wa wachezaji, kwa sababu sisi bado ndio klabu yenye ushindani mkubwa duniani.

"Kama nilivyosema awali na nilivyosema mara nyingi tunamuunga mkono kwa nguvu zote Ole ili kushinda mataji. Na huo ndio mpango wetu kama klabu."

United walikuwa nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu na bado walikuwa kwenye mshindano ya Ligi ya Europa na FA, wakati ligi ikisimama mwezi uliopita.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ALONSO AKARIBIA KUTUA MAN CITY

## ●●● Kwa ajili ya kuwa msaidizi wa Guardiola ambaye alikimbiwa na Arteta aliyejiunga na...

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa zamani wa Liverpool, Xabi Alonso anatajwa ni mmoja wa makocha wenye nafasi ya kutangazwa kuwa Kocha Msaidizi wa Pep Guardiola katika kikosi cha Manchester City.

Bado Guardiola amekuwa akitafuta kocha msaidizi mpya kwa ajili ya kurithi mikoba iliyoachwa na Mikel Arteta, ambaye aliondoka klabuni hapo Desemba mwaka jana na kujiunga na Arsenal kama Kocha Mkuu.

City inajiandaa kumtangaza mrithi wa Arteta katika kipindi cha majira ya joto, na taarifa zilizoandikwa na Goal zinasema, Alonso ndiye anayepewa nafasi kubwa ya kupewa kibarua hicho, huku Mhispania huyo aliwahi kufundishwa na Guardiola katika kikosi cha Bayern Munich.

Rodolfo Borrell, ambaye yuko katika sehemu ya benchi la ufundi la City, anatajwa anaweza kuchukua mikoba hiyo, lakini inaonekana kwamba klabu inahitaji kuajiri kocha kutoka nje.

**Kwa sasa Alonso ni kocha wa kikosi cha Real Sociedad B, ambaye ameiongoza timu hiyo kuwa katika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Daraja la Tatu Hispania.**

Awali alipata uzoefu wa kufundisha akiwa na kikosi cha timu ya vijana ya umri chini ya miaka 14 ya Real Madrid (U-14).

Mwaka 2018, Alonso alitembelea uwanja wa mazoezi wa City kwa lengo la kujifunza mbinu mbalimbali za ukocha za klabu hiyo.

Alonso alifundishwa na Guardiola alipokuwa mchezaji wa Bayern kati ya mwaka 2014 na 2016, na katika kipindi hicho, klabu hiyo ya Ujerumani ilitwaa mataji mawili ya ligi na Kombe la DFB-Pokal.

Akizungumza na vyombo vya habari Novemba mwaka jana, Alonso aliweka wazi aliamua kuondoka Real Madrid na kujiunga na Bayern mwaka 2014 kwa sababu alitaka kupata uzoefu wa kucheza akiwa chini ya Guardiola.

Alonso aliiambia The Athletic: "Nilikuwa na hali tofauti baada ya kubaini siri za Guardiola. Alikuwa akifundisha kwa mbinu halisia. Msimu wa soka ni mrefu lakini hadi tunafika mwisho, chini ya Pep huwezi kuchoka.

"Alitutahadharisha, kila siku alikuwa tayari. Kwa wachezaji, huenda hii ilitujenga na kutupa nguvu mpya kwenye miguu yetu wakati tunapoonekana tumezidiwa."

Makocha wengine ambao walikuwa na nafasi ya kuchukua mikoba ya Arteta ni pamoja na David Silva na Andres Iniesta, lakini nyota hao hawawezi kutokana na sasa bado wanacheza.

## KWA UFUPI

### POCHETTINO KUULA

KOCHA Mauricio Pochettino ndio chaguo la kwanza la wamiliki wapya wa Newcastle ili kurithi mikoba itakayoachwa na Steve Bruce, na wameweka wazi wako tayari kumlipa mshahara wa pauni milioni 19 kwa mwaka. (Sky Sports)

### BAYERN YAMTAKA SANE

KOCHA wa Bayern Munich, Hansi Flick alitumia dakika 30 kuzungumza katika simu na winga wa Manchester City na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Leroy Sane (24), kujadili suala la uhamisho wake mara dirisha la usajili litakapofunguliwa. (Bild, via Goal - in German)

### UNITED YAMTEGA SANCHO

WINGA wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho, ambaye ana umri wa miaka 20, ameahidiwa kupewa jezi namba saba katika kuongeza ushawishi wa nyota huyo kujiunga na Manchester United. (Mirror)

### NDOMBELE ANUKIA BARCA

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Tanguy Ndombele, anajiandaa kufahamu hatima yake ndani ya kikosi cha Tottenham, huku Barcelona inatajwa kuanza kuwania saini ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 23. (Sky Sports)

### PEDRO AKARIBIA ROMA

KOCHA wa Roma, Paulo Fonseca ameweka wazi nia yake ya kumsajili winga wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Hispania, Pedro, ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 32. (Corriere dello Sport - in Italian)

### CELTIC KUIKAMUA ARSENAL

ARSENAL imeambiwa ijiandae kutoa zaidi ya pauni milioni 25 kama inataka kunasa saini ya mshambuliaji wa Celtic Mfaransa Odsonne Edouard, ambaye ana umri wa miaka 22. (Express)

### MADRID, ARSENAL WATETA

ARSENAL imeanza mazungumzo na Real Madrid ili kujadili usajili wa beki wa kushoto wa Timu ya Taifa ya Hispania, Sergio Reguilon. Beki huyo mwenye umri wa miaka 23 kwa sasa yuko kwa mkopo katika klabu ya Sevilla. (ABC, via Star)

### FOFANA AINGIA SOKONI

MABOSI wa Leicester wameanza mchakato wa kumsajili beki wa kati wa Saint-Etienne Mfaransa Wesley Fofana, ambaye ana umri wa miaka 19. (Le10 Sport - in French)

### MILAN KUMUUZA REINA

AC Milan inajiandaa tena kufanya mchakato wa kumuuza golikipa wa zamani wa Timu ya Taifa ya Hispania, Pepe Reina mara dirisha la usajili litakapofunguliwa. Mlinda mlango huyo mwenye umri wa miaka 37 anaitumikia kwa mkopo klabu ya Aston Villa. (Calciomercato)

### PEARSON BADO YUPO

NIGEL Pearson ataendelea kuwa Kocha Mkuu wa Watford mpaka mwishoni mwa msimu huu endapo ligi itarejea, licha ya mkataba wake wa sasa kumalizika mwezi huu. (Sky Sports)

### ARSENAL MTEGONI

ARSENAL itajipanga kusajili wachezaji waliokuwa huru au kubadilishana nyota wake na klabu nyingine mara dirisha la usajili la majira ya joto litakapofunguliwa na uamuzi huu unasababishwa na tatizo la kifedha lililotokana na maambukizi ya virusi vya corona (COVID 19). (Mail)

HABARI MICHEZO

# NDASSA ALIKUWA KIUNGO KATIKA MUZIKI WA DANSI

**Na Sabato Kasika**

NI msiba jamani! Hadi majira ya juzi saa tano asubuhi, ndizo taarifa zilizotawala nchi nzima, hususan katika ulimwengu wa mtandao. Si mwingine, bali ni Mbunge wa Sumve, Richard Ndassa.

Ndassa huyu mbunge, hapo ni sehemu moja inayomhusu, lakini nyayo za umaarufu wake, zinagusa idara nyingine katika maisha ya kawaida.

Muda umepita na inawezekana wengi wakamfahamu katika sura ya kisiasa, ubunge, maana kutumikia robo karne si haba, waliozaliwa wakati anaanza, leo hii ndiyo vijana mitaani, kwenye ajira, mashambani, watafuta kazi na ambao vikao vyao vya harusi vinaendelea sehemu mbalimbali.

Kurudi kabla ya hapo, mathalani kwenye sekta yetu ya habari, ni mwenyeji kindakindaki akiwa na mzizi mrefu, ni meneja matangazo wa lililokuwa gazeti kubwa nchini. Ilikuwa kawaida, ukiingia katika ofisi za gazeti la Mfanyakazi, lililomilikiwa na Jumuiya ya Wafanyakazi Tanzania, eneo la Mnazi Mmoja, katika ghorofa ya kwanza kulia mwa kiti cha mhariri mkongwe, James Nhende ndiko alipopatikana Ndassa, wakati wote.

Tukirudi katika maisha ya kijamii, na hususan muziki wa dansi nchini, hadi umauti unamkuta, amekuwa mdau wa chanda na pete anayejulikana vyema kuanzia kwa ndugu zake wa habari, wanamuziki ndiyo usiseme, lakini zaidi ya hapo ameshawahi kubeba haiba ya mmiliki.

Kwa wanaofuatilia muziki wa dansi za zamani nchini unaotawala katika redio za nchini, hususan katika siku za mwisho wa wiki, hata kwa marejeo ya wiki moja iliyopita, ni mdau mkubwa wa kupiga simu kupongeza, kuchagua vibao au 'kutumbukiza' hili na lile kwa weledi kuhusu vibao vinavyopigwa na vituo vya hapa nchini.

Kwa kurejea nyuma kabla ya kuvaa wajihi wa ubunge, zama ambazo 'Dar inachemka kama bahari' dansi limetawala kila mahali, kumkosa Ndassa mahali hapo walau siku moja, katika mazingira ya kawaida pasipo dharura yoyote, msamiati 'haiwezekani' ni wa lazima. Naam! Hiyo ndiyo haiba yake kwa muziki.

Uswahiba wake kuanzia na bendi za muziki wa dansi, pia mwanamuziki mmoja mmoja ulikuwa juu kupindukia. Itakumbukwa, mapema miaka 1990, makazi yake yaliyopo Manzese Ukombozi, jijini Dar es Salaam, yaligeuka kuwa kijiwe maarufu cha wanamuziki.

Nakumbuka vyema, baadhi ya wanamuziki, wengine kadhaa wameshatangulia mbele ya haki, kama waimbaji maarufu mapacha raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Kasoloo Kyanga na Kyanga Songa, pia kaka yao ambaye anaimba na sasa yupo nchini Kenya, Skassy Kasambula, palikuwa kama nyumbani kwao.

Wakongo wengine, magwiji wapiga gitaa la solo maarufu katika bendi ya Maquiz, Nguza Vikings aliyepo nchini na mrithi wake, Vumbi Dekula Kahanga, anayeendeleza jukumu ughaibuni, daima hawakukosekana hapo Manzese Ukombozi.

Ni simulizi zinazowafikia wengi kama aliyekuwa bingwa wa kucharaza kinanda, marehemu Asia Daruweshi 'Super Mama', pia mwimbaji na mtunzi mahiri, Zahir Ally Zorro. Ndiyo picha halisi mahali hapo palivyokuwa kijiwe kamili cha muziki wa dansi na mara zote ukiwakuta hapo, basi wanabadilishana mawazo kuhusu mwenendo na ujuzi wa dansi, hata walifanya mazoezi.

Haikushangaza kushuhudia rasmi mwaka 1994, Ndassa huyo alipoanzisha bendi yake aliyoipa jina la Ngorongoro Heroes, hata pale ilipofyatua vibao iliibua mtikisiko mikubwa ndani ya tasnia hiyo. Sehemu kubwa ya majina yaliyoshuhudiwa kubadilishana mawazo kijiweni Manzese, Ukombozi, ndiyo safari hii walikamata vifaa vya bendi stejini wakimwaga burudani,

Hata hivyo, kama zilivyo bendi nyingine, Ngorongoro Heroes baadaye ilisambaratika, lakini Ndassa aliendelea kuhudhuria maonyesho ya muziki wa dansi kama kawaida na wanamuziki wakimtaja jina mara tu wanapomwona anaingia ukumbini, huku mwenyewe akiinua mikono juu au kupiga makofi.

Mungu ailaze roho ya Ndassa mahali pema, peponi, Amen.



Wanariadha kutoka sehemu mbalimbali wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA : JUMANNE JUMA** .

# Mbao yasubiri hatima ya Ligi

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Mbao FC umesema wapo tayari kupokea uamuzi wowote utakaotolewa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kuhusiana na hatima ya Ligi Kuu Bara msimu 2019/20.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Mbao FC, Richard Athanas alisema wanaangalia zaidi afya ya wachezaji na wadau wote wa soka, hivyo kuendelea kwa ligi bila mashabiki itakuwa ni adhabu kwa timu zinazoshiriki.

Athanas alisema licha timu yao kuwa katika nafasi mbaya ya kushuka daraja, bado wanaomba Bodi ya Ligi kuangalia hali ya maambukizi ilivyofikia na kamwe isichukue uamuzi kwa kukurupuka. "Kwa upande wetu Mbao tunajali afya za watu, kutokana na hali ya ugonjwa wa corona tungependa kuona viongozi wanalichukulia kwa upana, hakuna haraka ya kucheza mechi kama hali itazidi kuwa hatarishi, tutashauri ligi ifutwe kwa kufuata vigezo, maana hatujui ugonjwa huu unaisha na tayari baadhi ya mataifa yamefuta ligi zao," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza endapo TFF itachukua uamuzi wa kufuta Ligi Kuu, kwanza itatakiwa kuzingatia maslahi na haki za timu ambazo zilikuwa zinaburuza mkia kwenye msimamo.

Hata hivyo, katibu huyo alisema uvumilivu unahitajika zaidi wakati huu ili uamuzi wowote utakaochukuliwa, usilete madhara kwa upande wowote.

## Kagere 'amnyima usingizi' Sonso

**Na Shufaa Lyimo**

BEKI wa Yanga, Ally Sonso amesema huwa 'hapati usingizi' kila anapokutana na mshambuliaji wa mabingwa watetezi na vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Meddie Kagere.

Akizungumza na gazeti hili Dar es Salaam jana, Sonso alisema anavutiwa na kiwango alichonacho Mnyarwanda huyo na kukiri ana sifa zote za kuwa mshambuliaji.

"Namkubali Kagere kwa sababu ni mshambuliaji ambaye anatumia nguvu na mbio anapokuwa uwanjani, hivyo nikikutana nae huwa ananiumiza kichwa," alisema Sonso.

Beki huyo alisema Kagere ni mshambuliaji ambaye anajituma na kutochagua mechi kama ilivyo kwa wachezaji wengine nyota waliowahi kucheza Ligi Kuu Bara na hali inayomfanya aige mfano wake.

"Namheshimu, kila siku napenda aina ya uchezaji alionao, anasifa zote za kuwa mchezaji wa kimataifa," Sonso alisema.

Aliongeza kuwa katika kipindi hiki cha mapumziko, anaendelea kujiimarisha kwa kufanya mazoezi ili watakaporejea uwanjani awe na kiwango bora cha kuisaidia timu yake kupata ushindi.

## Kipanga yafikiria ubingwa Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MABOSI wa Kipanga inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar wamesema bado hawajakata matumaini ya kutwaa ubingwa wa ligi hiyo, endapo itarejea tena kumalizia mechi zilizosalia za msimu wa 2019/20, imefahamika.

Katibu Msaidizi wa Kipanga, Maulid Othman, alisema matarajio ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara yalirejea baada ya kushinda michezo yake saba mfululizo ambayo walicheza kabla ya kusimama kwa ligi hiyo na kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo.

Othman alisema ushindi huo umeamsha matumaini mapya kuanzia kwa wachezaji na viongozi wa timu hiyo ambao wanaendelea 'kuisuka zaidi' ili malengo waliyonayo ya kuchukua taji yatimie.

"Tunamatumaini makubwa ya kuchukua ubingwa wa msimu huu, tulishinda mechi mfululizo na hali hii imetupa nguvu zaidi, kutoka nafasi ya 15 hadi ya saba katika msimamo, tutapambana ili malengo yetu yatimie," Othman alisema.

Kipanga ipo nafasi ya saba katika Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na pointi 28 baada ya kucheza michezo 20.

Michezo
Ijumaa Mei 1, 2020
Nipashe

Alonso akaribia kutua Man City



HABARI UK.22

# KARIA: DK. MENGI ALITAKA KUIONA STARS QATAR 2022

●●● Shirikisho hilo limeweka wazi ndoto hiyo inawasumbua na wanajipanga kuhakikisha...



Mwenyekiti Mtendaji wa IPP na mlezi wa Timu ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), Dk. Reginald Mengi (kulia), akisalimiana na Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia. **PICHA: MAKTABA**

**Na Somoe Ng'itu**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), ni moja ya taasisi mbalimbali za hapa nchini ambazo zilifanya kazi kwa karibu na Dk. Reginald Abraham Mengi.

TFF ilishirikiana na Dk. Mengi katika kuhakikisha Timu ya Soka ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys) iliyokuwa imefuzu kushiriki katika fainali za Afrika (AFCON U-17) zilizofanyika Aprili mwaka jana, inajiandaa vema na kupeperusha vizuri bendera ya Tanzania.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam, Rais wa TFF, Wallace Karia, alisema changamoto kubwa waliyonayo ni kuhakikisha Timu ya Taifa (Taifa Stars), inakata tiketi ya kushiriki katika fainali zijazo za Kombe la Dunia zitakazofanyika Qatar mwaka 2022.

Karia alisema kuwa TFF inajipanga kuhakikisha wanakamilisha ndoto hiyo ya kuipeleka Taifa Stars katika fainali hizo kwa mara ya kwanza ili kumuenzi kwa vitendo Mkurugenzi Mtendaji wa IPP.

Rais huyo alisema kama Taifa Stars itafanikiwa kutinga katika fainali hizo, hakika mdau huyo atakuwa ameenziwa vema.

Alisema hata kama Taifa Stars haitapata nafasi ya kushiriki katika fainali hizo zinazoandaliwa na Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), angependa kuona timu hiyo inafika mbali kwenye safari ya kuelekea katika michuano hiyo mikubwa duniani.

"Kuna kauli Dk. Mengi aliwahi kusema na ambayo hatuwezi kuisahau ni ndoto yake kubwa kuona Stars inakwenda katika fainali za Kombe la Dunia Qatar 2022, hiyo ni changamoto kubwa ametuachia inayotusumbua akilini, basi hata kama hatutafuzu, angalau tufanye vizuri na kutolewa hatua za mbele," alisema Karia.

**Kiongozi huyo alisema Dk. Mengi alikuwa na ndoto za kuiona Serengeti Boys inafanya vizuri katika mashindano mbalimbali inayoshiriki na aliwataka wachezaji wa timu hiyo wafikirie kucheza mpira tu.**

Alisema kufariki kwa Dk. Mengi ni pigo kubwa katika familia ya mpira wa miguu na ili kuhakikisha wanamuenzi kikamilifu ni kuendeleza mazuri katika timu zote za Taifa.

"Tunajukumu la kumuenzi vizuri Dk. Mengi, hili kwetu ni deni," alimaliza Karia.

Dk. Mengi ambaye alikuwa mlezi wa Serengeti Boys, alisema ana imani timu hiyo itatoa wachezaji nyota ambao kwa kushirikiana na nyota wengine wazoefu, watakwenda katika fainali za Kombe la Dunia za Qatar.

"Alikuwa akiwalea kama wajukuu zake, aliwataka kufikiria kucheza mpira tu, na aliwaambia wamuombee asifilisike," alisema Karia.

**NUKUU ZA DK. MENGI**

"Nina imani na timu hii, inaweza kuipa Tanzania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika Qatar mwaka 2022, na zile za mwaka 2026 zitakazochewa Marekani, Mexico na Canada.

"Sisi tutajipanga kushinda nchi zote nane, kushinda mechi zote nane, Tanzania ina uwezo wa kushinda Kombe la Dunia, tunatakiwa tujiamini kuwa tutashinda, hatutaki kushinda mechi tatu, tunataka kushinda mechi zote, tunataka kushinda kila mashindano tutakayoshiriki."

"Timu ya Serengeti Boys ni timu ya washindi, tunataka Watanzania tupate sifa ya kushiriki Kombe la Dunia, hakuna sababu ya kushindwa, tunatakiwa tujiamini, tutawashangaza, tuko hapa kuwaambia Watanzania tunaweza, tunataka kila mechi iwe ya hapa Dar es Salaam au nje, tukienda uwanjani tujue tutashinda, kwa sababu tunaweza."

"Huu ni mwaka wa Watanzania, tunaweza kwenda Kombe la Dunia, huu ni wakati wa Tanzania...tutafanya kila tuwezalo, tutawapa malezi mazuri wachezaji wetu, nina imani na vijana hawa, tunaweza."

## Mwamnyeto ajipanga kuwabeba Watanzania

**Na Saada Akida**

WAKATI vigogo wa soka nchini, Simba na Yanga wakiendelea kupigana vikumbo kuwania saini ya Bakari Mwamnyeto, beki huyo wa kati wa Coastal Union, amesema anataka kuona usajili wake unaleta mapinduzi kwa wachezaji wazalendo.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwamnyeto alisema ataongeza umakini katika mchakato huo wa usajili kwa sababu anataka kuona thamani ya wachezaji Watanzania pia inapanda.

Mwamnyeto alisema bado hakuna klabu ambayo ameshafikia nayo makubaliano na sasa yuko jijini Tanga akiendelea kujifua huku akisubiri taarifa mpya ya hatima ya Ligi Kuu Bara kutoka katika Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

"Soka ndio kazi yangu, nitaangalia zaidi maslahi, kwa maana hiyo, yoyote atakayekuja na ofa nzuri sawa, pia klabu hizi zinatakiwa kuthamini wachezaji wazawa katika suala la usajili," alisema Mwamnyeto.

Alisema klabu itakayokuwa tayari kumlipa ada ya Sh. milioni 90 na mshahara wa Sh. milioni tano kwa mwezi, ndiyo itakayopata saini yake na ataitumikia kwa uadilifu wa hali ya juu.

Mwamnyeto ameonyesha kiwango kizuri msimu huu na kuisaidia Coastal Union kufanya vema huku pia akiwa mlinzi tegemeo katika kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars).

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002